**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

---

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**ILIYOWASILISHWA NA**
**MHESHIMIWA HEMED SULEIMAN ABDULLA MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR**

***ZANZIBAR***

***6 MEI, 2026***



**MHESHIMIWA HEMED SULEIMAN ABDULLA**

**MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR**



**MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA,**
**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,**
**(SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI)**



**DKT. ISLAM SEIF SALUM**
**KATIBU MKUU OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**



**NDG. SALHINA MWITA AMEIR, NAIBU KATIBU MKUU OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

## *Dira*

***" Kuwa na Serikali yenye kutoa huduma bora kwa jamii na yenye uhimili mzuri wa uchumi, umoja na maendeleo endelevu"***

## Dhamira

***"Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali katika sekta zote za SMZ na masuala ya Muungano kwa kufuata misingi ya Katiba na Sheria pamoja na kufuata misingi ya haki za binaadamu na ushirikishwaji".***

**HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika;** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na hatimae likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika;** kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kukutana hapa leo katika tukio hili muhimu tukiwa na amani, mshikamano na utulivu katika nchi yetu. Tumuombe Mwenyezi azidi kuilinda amani yetu, awalinde viongozi wetu na wananchi wote na atupe hekima na baraka katika maamuzi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika;** kwa dhati kabisa napenda kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoliongoza vyema Taifa letu kwa kuleta maendeleo kwa wananchi na kudumisha amani na Muungano wetu ambao kwa sasa umetimiza miaka 62 kwa mafanikio makubwa.

4. **Mheshimiwa Spika;** vile vile, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kushirikiana vyema na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kulinda tunu za Taifa letu, amani, umoja na Muungano wetu, sambamba na kutoa miongozo bora ya maendeleo ambayo matunda yake tunayaona kupitia miradi ya kimkakati kwenye sekta mbali mbali ikiwemo, Uwekezaji, Uchumi wa Buluu, uwezeshaji wananchi kiuchumi, usafiri na usafirishaji, biashara na huduma za kijamii kote nchini. Kwa hakika tunasema Dkt. Mwinyi, ni kiongozi anaeacha alama. Sisi wasaidizi wao tunawaahidi kuendelea kufuata na kusimamia ipasavyo maelekezo yao na kuhakikisha yanatafsiriwa kwa vitendo na kuleta matokeo chanya kwa wananchi na vilevile kunafikia lengo la Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030.

**5. Mheshimiwa Spika,** kadhalika, niendelee kwa kutoa shukrani za pekee kwako, Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri na uwezo wako mkubwa wa kusimamia shughuli za Baraza hili tukufu, jambo ambalo limeleta ufanisi wa hali ya juu katika utendaji wetu. Shukrani zangu na pongezi pia, nazitoa kwa Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano na usaidizi wao kwako Mheshimiwa Spika na kwetu sisi Wajumbe katika kuongoza mikutano na vikao. Bila shaka weledi na uzoefu wenu ndio umekuwa nguzo ya mafanikio ya Baraza hili katika kutekeleza majukumu yake ya kisheria.

**6. Mheshimiwa Spika**; napenda kutoa shukrani maalum kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Aza Januar Joseph, Mwakilishi wa Viti Maalum Wanawake na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kusimamia utekelezaji wa bajeti yetu ya Mwaka 2025/2026 na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya mwaka 2026/2027 na kuyapitisha yawasilishwe katika kikao hiki. Aidha, natoa pongezi kwa Wenyeviti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanayoifanya .

**7. Mheshimiwa Spika,** napenda pia, kuwapongeza sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuitumia vizuri nafasi zao kuwawakilisha wananchi na kuishauri vyema Serikali kupitia michango yao wanayoiwasilisha katika Baraza hili Tukufu na kuleta tija kubwa katika kuboresha huduma za kijamii kote nchini.

**8. Mheshimiwa Spika;** baada ya maelezo hayo ya utangulizi wa shukurani na pongezi, kwa ruhusa yako naomba nitoe muhtasari wa hali ya utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Serikali kwa kipindi cha 2025/2026 na mwelekeo wetu kwa mwaka 2026/2027 katika sekta za kiuchumi, kijamii na nyanja za kisiasa katika nchi yetu.

## MWENENDO WA UCHUMI WA ZANZIBAR

### Ukuaji wa Uchumi

**9. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka 2025 kasi ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar ni asilimia **7.0** ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia **7.1** mwaka 2024. Ukuaji huo umechangiwa na:

i. Kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya sekta ya kodi za bidhaa na huduma, ambapo kwa mwaka 2025 makusanyo ya kodi yameongezeka kwa wastani wa

asilimia **12.8** kutoka wastani wa asilimia **7.0** mwaka 2024;

ii. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii nchini kufikia watalii **917,167** mwaka 2025 kutoka watalii **736,755** mwaka 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 12.4;**

iii. Kuongezeka kwa miradi mipya ya uwekezaji kwa **asilimia 13.0** kufikia miradi **136** yenye thamani ya **Shilingi Trilioni 1.89** iliyosajiliwa mwaka 2025 kutoka miradi **131** yenye thamani ya **Shilingi Trilioni 1.88** iliyosajiliwa mwaka 2024; na

iv. Kuongezeka kwa ukuaji wa sekta ndogo ya Malazi na Chakula kwa **asilimia 17.5** mwaka 2025 kutoka **asilimia 16.9** ya mwaka 2024.

**10. Mheshimiwa Spika;** Kupungua kwa kasi ya ukuaji kwa asilimia 0.1 kumetokana na kupungua kwa ukuaji wa sekta ya kilimo ambayo inajumuisha sekta ndogo ya Mazao, Ufugaji, Misitu na Uvuvi kufikia asilimia 23.5 mwaka 2025 kutoka asilimia 24.3 mwaka 2024 pamoja na kupungua kwa ukuaji wa sekta ya viwanda ambayo inajumuisha sekta ndogo ya uchimbaji mawe na mchanga, ujenzi, umeme na gesi, uzalishaji viwandani na shughuli za usambazaji maji safi na kudhibiti maji machafu kufikia asilimia 19.3 mwaka 2025 kutoka asilimia 20.2 mwaka 2024.

**Pato Halisi la Taifa**

**11. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka 2025, Pato halisi la Taifa (Constant Prices) limeongezeka kufikia thamani ya **Shilingi Bilioni 4,307.9** ikilinganishwa na **Shilingi Bilioni 4,026.4** mwaka 2024. Wakati Pato la Taifa kwa bei za soko (Current Prices) limeongezeka kufikia thamani ya Shilingi **Bilioni 7,029.9** mwaka 2025 kutoka thamani ya **Shilingi Bilioni 6,572.6** mwaka 2024.

**Pato la Mwananchi**

**12. Mheshimiwa Spika;** kuongezeka kwa Pato la Taifa Zanzibar kumepelekea pia, kuongezeka kwa kipato cha Mwananchi. Kwa mwaka 2025, Pato la mwananchi limeongezeka na kufikia Shilingi Milioni 3.349 kutoka Shilingi Milioni 3.227 mwaka 2024.

**Mfumko wa Bei**

**13. Mheshimiwa Spika;** Kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2025 imepungua na kufikia wastani wa **asilimia 4.1** kutoka wastani wa **asilimia 5.1** mwaka 2024. Kupungua

huko kumetokana na kupungua kwa mfumko wa bei wa bidhaa za chakula katika soko ambapo kwa mwaka 2025 bidhaa za chakula zimepungua na kufikia wastani wa **asilimia 5.0** kutoka wastani wa **asilimia 8.4** mwaka 2024 kulikotokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani na Serikali kutoa ruzuku na kusimamia bei elekezi ilizozitoa kwa bidhaa za chakula.

Aidha, mfumko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula umefikia wastani wa **asilimia 3.4** mwaka 2025 kutoka wastani wa **asilimia 2.7** mwaka 2024 kulikosababishwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa duniani pamoja na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji.

**Hatua za Kudhibiti Mfumko wa Bei**

**14. Mheshimiwa Spika;** hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ili kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kama ifuatavyo:

i. Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;

ii. Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaendelea kufuatilia na kuchukua hatua za kudhibiti kushuka kwa thamani kwa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani;

iii. Kuimarisha ufanisi wa Bandari ya Malindi kwa ununuzi wa vifaa vya kisasa na kuimarisha bandari nyengine ili kupunguza muda wa kutoa mizigo bandarini; na

iv. Serikali kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini sambamba na kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku.

**Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2026**

**15. Mheshimiwa Spika;** mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2026 unakwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati (ZADEP II) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030, pamoja na Maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**16. Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa **asilimia 7.5** mwaka 2026 kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa **asilimia 9.3** kutoka watalii **917,167** kwa mwaka 2025 hadi watalii **1,002,917** mwaka 2026;

ii. Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara mjini na vijijini, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, Ujenzi wa Mji wa Serikali Kisakasaka, Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani, Bandari ya Mpigaduri na Ujenzi wa Mji wa Michezo (AFCON City) Fumba. Miradi mengine itakayochangia ukuaji wa uchumi ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama, umeme na ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila Wilaya;

iii. Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei ili kubakia katika tarakimu moja;

iv. Kuongezeka kwa uhamasishaji wa ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa matumizi ya Serikali;

v. Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza thamani na miradi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;

vi. Kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi kutokana na juhudi za Serikali za kukuza uwekezaji, uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira; na

vii. Kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ya uchumi wa buluu na kuimarisha matumizi endelevu ya bahari.

**17. Mheshimiwa Spika;** hata hivyo, kwa mwaka 2026 makadirio ya ukuaji wa uchumi yanaweza kuwa chini ya wastani wa **asilimia 7.5** ikiwa mgogoro wa vita baina Iran na Israel – Marekani utaendelea kudumu kwa muda mrefu kutokana na kuathiri baadhi ya shughuli kuu za uchumi duniani zikiwemo sekta ya utalii, usafirishaji, uwekezaji mitaji na biashara sambamba na kupanda kwa bei za mafuta ambazo zitaathiri uzalishaji wa ndani.

## MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI NCHINI

### Kuimarika kwa Sekta ya Kazi na Uwekezaji

**18. Mheshimiwa Spika;** Serikali imepiga hatua kubwa katika kuimarisha ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kwa kufanya mapitio ya maandiko ya miradi mipya **22,** ambapo miradi saba **(7)** tayari imeshatiwa saini. Vilevile, Serikali imeendelea kupiga hatua katika uendelezaji wa visiwa vidogovidogo vya kimkakati. Visiwa vitatu **(3)** tayari vimevutia uwekezaji kamili na ujenzi unaendelea katika visiwa vingine vitano **(5)** ili kuimarisha sekta ya utalii na uchumi wa buluu.

**19. Mheshimiwa Spika;** Serikali imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi **13** kati ya miradi **20** ya PPP kwa lengo la kutathmini utekelezaji wake. Tathmini imeonesha kuwa baadhi ya miradi imeanza kuendelezwa ikiwemo hatua ya ujenzi na mingine ipo katika hatua ya kutoa huduma ikiwemo Bandari ya Fumba, Bandari ya Malindi na Karakana Kuu ya Magari Zanzibar. Vilevile, Serikali imesajili miradi ya uwekezaji **92** yenye thamani ya Dola za Kimarekani **Milioni 561** kati ya Miradi **90** iliyokadiriwa kwa thamani ya **Dola Milioni 390.67** katika Sekta za Utalii, Real estate, Viwanda na Mifugo.

**20. Mheshimiwa Spika;** Serikali imefanya zoezi la ukaguzi na tathmini kwa ajili ya ulipaji fidia katika maeneo makuu sita ambayo ni Upanuzi katika eneo la Bandari ya Fumba; Ujenzi wa barabara za ndani **kilomita 8** katika eneo la Uwekezaji Fumba, Eneo la Mradi wa IIT Madrasa, Eneo la ujenzi wa Viwanja vya AFCON, Eneo la ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa na ICT park. Jumla ya **Shilingi Bilioni 2.365** zinahitajika kulipwa kwa wananchi watakaoathirika na Miradi hii ya Uwekezaji.

**21. Mheshimiwa Spika;** kwa lengo la kuendeleza shabaha ya sekta ya uwekezaji, Serikali imepanga kusajili miradi ya uwekezaji **110** yenye thamani ya **Dola Milioni 620** na kuzalisha ajira **2,100** kupitia mkakati wa masoko na ufuatiliaji wa miradi ya PPP, huku ikiimarisha mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa kazi.

Aidha, Serikali imejipanga kikamilifu kupitia maboresho ya kisheria, mifumo ya kidijitali, na miundombinu ya kisasa ili kuhakikisha uwekezaji unakuwa salama na wenye tija. Nitoe wito kwa sekta binafsi na jamii kwa jumla kuwekeza kwa wingi wakati tukiendelea kuweka mazingira rafiki, usalama wa mitaji yao na ushirikiano wa dhati katika kila hatua ya utekelezaji wa miradi yao.

**22. Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa kuimarisha soko la ajira na kulinda maslahi ya nguvu kazi nchini, Serikali imethibitisha jumla ya mikataba ya wafanyakazi **11,613** (Unguja **9,790** na Pemba **1,823**) ambapo wanaume ni **7,592** na wanawake ni **4,021** sawa na **asilimia 111** ya makadirio ya **10,500** kwa lengo la kuhakikisha masharti na viwango vya mikataba hiyo vinaendana na Sheria, Kanuni na Miongozo ya kazi iliopo Nchini. Sambamba na hilo Serikali imetoa vibali vya kazi kwa wageni **2,877** kutoka katika mataifa mbalimbali yakiwemo ya Italia, Ujerumani, Marekani, Uingereza, Uturuki, Ethiopia, India, China, Korea na Afrika ya Kusini.

**Uimarishaji wa Huduma za Maji, Nishati na Madini**

**23. Mheshimiwa Spika;** Katika kuimarisha huduma za usambazaji maji, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji Miundombinu ya Maji Kengeja – Pemba, uliotekelezwa na Mkandarasi Upstairs Engineering Ltd kutoka Tanzania. Mradi huu uligharamiwa na Serikali kwa kiasi cha **Shilingi 1,036,262,339** na umekamilika kwa mafanikio makubwa na umezinduliwa rasmi tarehe 02 Januari, 2026 katika Maadhimisho ya Miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**24. Mheshimiwa Spika;** Serikali kupitia ZAWA na Kampuni ya Rand Water, iliendelea na juhudi za kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini. Juhudi hizo ni pamoja na kurekebisha sehemu **89** zilizokuwa zikivujisha maji, yakiwemo mabomba makubwa ya usafirishaji maji majumbani, jambo ambalo limesaidia kupunguza malalamiko ya wananchi juu ya upatikanaji wa huduma ya maji na pia, kuokoa maji mengi yaliyokuwa yakipotea.
Aidha, kazi ya uwekaji wa mabomba mapya ya kisasa ya HDPE yenye urefu mita **48** imefanyika katika maeneo ya Mkoani na Mvumoni Pemba, pamoja kuweka mtandao mkubwa wa mabomba mapya katika kisiwa cha Unguja wenye urefu wa **kilomita 15.** Vilevile, Visima **8** kwa Pemba na Visima **6** kwa Unguja vilisafishwa, pump **8** zilikarabatiwa Pemba na pampu **7** mpya zilifungwa Unguja.

**25. Mheshimiwa Spika;** Serikali imeendelea na jukumu lake la kuzalisha, kusambaza na kuuza umeme kwa wananchi wa Zanzibar kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO). Serikali imepata mafanikio makubwa katika sekta hii ya umeme kwa kukusanya mapato ya S**hilingi 118,946,731,496.43** ikiwa ni asilimia **86** ya makadirio na kuunganisha wateja wapya **20,337** ikiwa ni **asilimia 105** ya makadirio. Vilevile, juhudi za kueneza nishati vijijini zimefikia **asilimia 91** kwa kuunganisha vijiji **20** kati ya **22** vilivyopangwa. Miongoni mwa vijiji vilivyounganishiwa umeme ni Muyuni C, Uzi Shamba, Jambiani Mashambani, Chaani Ketwa, Kizimkazi, Hanyegwa Magurueni,

Cheju, Pete, Muyuni A, Jendele Maguruweni, vijiji vya Kidoti, Kijibwe Mtu, Bwejuu Mashambani kwa Unguja na Mjini Wingwi, Kwa Mgogo Sipwese, Momoni na Rasi Gando kwa Pemba.

**26. Mheshimiwa Spika;** Aidha, miundombinu ya huduma ya umeme imeimarishwa zaidi kupitia ufungaji wa nguzo **1,140** (Unguja **652,** Pemba **488**), ukaguzi wa transfoma **497** na kusawazisha umeme katika maeneo **23** ili kuondoa changamoto ya umeme mdogo.

**27. Mheshimiwa Spika;** Kazi ya uendelezaji wa miradi ya kimkakati ya ZESTA (Lot I: 42.6%, Lot II: 59.2%) inaendelea vyema sambamba na kuendelea na maandalizi ya mradi wa waya wa baharini (Submarine Power Cable) wa **220KV (MW 270).** Hatua hizi zinaenda pamoja na uwekezaji katika nishati jadidifu kupitia miradi ya Solar PV Makunduchi na Matemwe pamoja na mifumo ya kisasa ya kuhifadhi nishati BESS, ikilenga kuleta uhakika wa nishati nchini.

**28. Mheshimiwa Spika;** Mafanikio haya makubwa ni matokeo ya utekelezaji madhubuti wa sera na mikakati ya Serikali chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kukabiliana na changamoto zilizopo, ikiwemo miundombinu chakavu na uhaba wa rasilimali, kupitia uwekezaji wa kimkakati na uandaaji wa sheria na miongozo mipya. Vilevile, Serikali itaendelea kutilia mkazo ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, kwa kuongeza kasi ya kutoa huduma bora, endelevu na za uhakika ili kuchochea ustawi wa huduma za kijamii na ukuaji wa uchumi wa Zanzibar kwa ujumla.

**Ukuaji wa Sekta ya Utalii**

**29. Mheshimiwa Spika;** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kuchukua jitihada kubwa katika kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi. Jitihada hizo zimepelekea ongezeko kubwa la idadi ya watalii wanaoingia nchini. Idadi ya watalii walioingia Zanzibar mwaka 2025 imefikia **917,167,** ikilinganishwa na watalii **736,755** mwaka 2024, sawa na ongezeko la **asilimia 24.5**. Pia, idadi ya siku za ukaazi kwa mtalii zimeongezeka kutoka siku **7** mwaka 2022 hadi siku **8** mwaka 2025.

**30. Mheshimiwa Spika;** Serikali kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Uchumi Barani Afrika (UNECA) imeandaa Mfumo wa Upimaji wa Mchango wa Utalii kwenye Pato la Taifa (Tourism Satellite Account). Kukamilika

kwa mfumo huu kumewezesha kujulikana mchango halisi wa utalii katika pato la taifa na tayari ripoti hiyo imeshatolewa na imeshaanza kutumika ambapo kwa sasa ni **asilimia 29.2.** Aidha, Kuanzia mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara inayohusika na Utalii itandelea na mchakato wa kupima mchango wa sekta ya Utalii katika uchumi kila mwaka.

**31. Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Zanzibar imefanikiwa kutunukiwa tuzo ya "Africa Corporate Retreat Destination", jambo linalodhihirisha ushindani wake na ubora wake ikilinganishwa na maeneo mengine ya utalii barani Afrika. Kupatikana kwa tuzo hii kumechangia kuitangaza zaidi Zanzibar kitaifa, kikanda na kimataifa na hivyo kuchochea ongezeko la idadi ya watalii wanaoitembelea.

**32. Mheshimiwa Spika;** Serikali itaendelea kuimarisha Sekta ya Utalii kupitia miradi ya kimkakati ikiwemo, ZanziLand Theme Park, Zanzibar Aquarium na ujenzi wa miundombinu ya kisasa ikiwemo Sea Taxi Marinas, huku ikihakikisha uhifadhi wa Mji Mkongwe kupitia ukarabati wa majengo ya kihistoria kama vile Beit el Ajaib. Vilevile, Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha utalii kwa wote pamoja na kukiimarisha Chuo cha Utalii (ZITOD) kuwa kituo cha umahiri (centre of excellence) ili kuzalisha rasilimali watu yenye ushindani wa kimataifa. Aidha, Serikali itahuisha akaunti ya satelaiti ya utalii (TSA) na kutekeleza mkakati mpya wa chapa ya utalii (Zanzibar Tourism Brand) ili kuongeza muonekano wa Zanzibar na kuvutia masoko mapya ya watalii na wawekezaji.

**Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi na Uimarishaji wa Makaazi**

**33. Mheshimiwa Spika;** Serikali imepiga hatua kubwa katika kusimamia matumizi ya ardhi kwa kurasimisha miliki za ardhi kwa kutayarisha jumla ya hati **1,319** za haki ya matumizi ya Ardhi (**600** kwa Unguja na **719** Pemba) pamoja na kufanya uhakiki wa hati **308** (**167** Unguja na Pemba hati **141**). Vilevile, Serikali imetayarisha jumla ya Mikataba **209** (**190** kwa Unguja na **19** Pemba) ya Ukodishwaji wa Ardhi na kufanya ukaguzi wa maeneo **252** kwa Unguja na **143** Pemba, jumla ya Mikataba **100** (mikataba **74** kwa Unguja na **26** kwa Pemba) ya Ukodishwaji wa Ardhi imefanyiwa uhakiki.

**34. Mheshimiwa Spika;** Serikali imeendelea na zoezi la upimaji wa ardhi ambapo jumla ya viwanja **84** vya Serikali na viwanja **1,206** vimepimwa kutokana na maombi ya wananchi. Kadhalika, Serikali imetayarisha jumla ya hati 440 za Mashamba ya Eka Tatu, kufanya ukaguzi wa maeneo **655** (Unguja **502** na **153** Pemba), pamoja na kufanya kazi **777** za uthamini ambazo kwa upande wa Unguja ni **511** na kwa Pemba **266.**

**35. Mheshimiwa Spika;** katika kuimarisha usajili wa makaazi, Serikali imepiga hatua kubwa katika usimamizi wa Kondominio Unguja na Pemba, ambapo jumla ya fomu **187** za maombi ya usajili zimetolewa. Pia imesajili ramani saba **(7)** kwa miradi ya Kondominio ambayo ni AMG Company limited uliopo Michamvi, The System Design Solutions (Phase 3) uliopo Mbweni, TMA Holdings Company limited uliopo Nungwi, JNB Zanzibar Limited uliopo Kiwengwa, Sharban Jusab Tharia uliopo Mkunazini, HM Camaradas (Spectral Invest Limited as Developer) uliopo Paje na Itaset Company limited (Yako Hospitality Limited as Developer) uliopo Kiwengwa.

**36.Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali inaendelea na hatua za kimkakati za uandaaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi katika Kisiwa cha Pemba ambao unaenda sambamba na utayarishaji wa mipango kwa miji minne **(04)** ya Chake-chake, Wete, Mkoani, na Micheweni. Kwa sasa mshauri elekezi anakamilisha rasimu ya awali ya Mpango huo. Pia, juhudi za kuimarisha viwango vya ujenzi nchini zinaendelea kwa kuandaa Miongozo ya Ujenzi (Building Codes) ili kuhakikisha usalama na mpangilio bora wa makaazi na majengo Zanzibar.

**37. Mheshimiwa Spika;** miradi mikubwa ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa Ofisi ya Shirika la Nyumba Pemba na jengo la Makaazi na biashara la gorofa 5 Kiembe samaki ambalo lina nyumba **22** umekamilika na kuzinduliwa rasmi katika Sherehe za Miaka 62 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

**38. Mheshimiwa Spika;** katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya makaazi bora, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya makaazi na biashara ikijumuisha ujenzi wa jengo moja la nyumba **22** za makaazi Mombasa – kwa Mchina (Phase II) ambao umefikia **asilimia 48.** Pia, ujenzi wa jengo la biashara Maisara (**2** Tower Golf Club) Unguja umeanza kwa hatua za awali na kufikia **asilimia 3** ya utekelezaji wake. Vilevile, ujenzi wa Nyumba **1,095** awamu ya kwanza Chumbuni unaendelea vyema na hivi sasa umefikia **asilimia 20.**

**39. Mheshimiwa Spika;** maeneo mengine ya ujenzi wa kimkakati ni pamoja na ujenzi wa nyumba **548** za Makaazi na Biashara Kisakasaka 'B' (phase I) umeanza; ujenzi wa nyumba **288** za Makaazi na Biashara Kisakasaka 'C' upo katika hatua ya manunuzi; na ujenzi wa nyumba **312** za Makaazi na Biashara Kisakasaka 'D' unaendelea na umefikia **asilimia 7.** Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba **8** Mkungu Malofa Chake Chake Pemba awamu ya pili; Mradi wa ujenzi wa nyumba **250** za makaazi Wete-Polisi Line na Ujenzi wa nyumba **100** za Watumishi wa Umma kwa kila Wilaya Unguja na Pemba.

**40. Mheshimiwa Spika;** wito wangu kwa wananchi wote kuhakikisha wanatumia ardhi kwa kufuata mipango ya matumizi ya ardhi iliyowekwa na mamlaka husika na kuepuka ujenzi holela, huku tukihimiza ujenzi wa majengo ya ghorofa (Kondominio) ili kuokoa rasilimali ardhi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii. Ni vyema kila mwananchi akazingatia umiliki wa hati rasmi, pamoja na kushirikiana na mamlaka katika kurasimisha na kupima viwanja ili kudhibiti na kumaliza migogoro ya ardhi. Hii itasaidia kuhakikisha Zanzibar inastawi kupitia makaazi bora, salama na yenye muonekano mzuri kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**41. Mheshimiwa Spika;** Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya uwezeshaji kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa mifumo tofauti. Serikali imevipatia vikundi vya vijana **24** ruzuku yenye thamani ya **Shilingi 21,591,553,** vifaa na mafunzo ya ujasiriamali na masoko ya kidijitali. Sambamba na kuwapatia programu za stadi za maisha, uongozi na uraia ambazo zimewafikia vijana **9,329** (wanawake **5,195,** wanaume **4,134)** kupitia waelimishaji rika **80** na makongamano ya kitaifa. Pamoja na kutoa mafunzo ya vitendo na kitaaluma kwa vijana **2,513** katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, afya, TEHAMA, usalama barabarani na uchumi wa buluu ili kuongeza ajira na ujuzi.

**42. Mheshimiwa Spika;** Katika kuendeleza sekta ya ushirika nchini, jumla ya Vyama vya Ushirika **968** vilifanyiwa ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa kawaida na kubaini changamoto za kifedha, utawala na uendeshaji na kupewa ushauri wa kitaalamu. Aidha, jumla ya Vyama **1,071** (Unguja **660,** Pemba **411**) vilisajiliwa na kufanya idadi ya Vyama vya Ushirika kufikia **7762** (Unguja **3906** na Pemba **3,856**). Serikali imetoa mafunzo ya uongozi, usimamizi wa fedha na ujasiriamali kwa wanachama **5,478** kutoka Vyama vya Ushirika **887** kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya ushirika. Kwa upande wa mikopo Serikali imetoa mikopo yenye jumla ya **Shilingi 12,739,637,966** kwa wanufaika **6,578** (wanawake **5,944** na wanaume **634**).

**43. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha utendaji wa Mabaraza ya Vijana ili kukuza ushiriki wao katika fursa za kitaifa na kimataifa ikiwemo ajira. Serikali itaendelea kuratibu upatikanaji wa ajira za staha **140,000** ifikapo mwaka 2027. Aidha, serikali imepanga kuvipatia vikundi vya kijamii **7,000** mikopo nafuu, mafunzo ya ujasiriamali, na ukuzaji wa masoko ili kuweza kuanzisha na kuendeleza shughuli za kiuchumi zitakazowanufaisha kimaisha.

**44. Mheshimiwa Spika;** napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa wananchi hususan vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, kuchangamkia fursa mbalimbali za uwezeshaji zinazotolewa na Serikali na wadau wake kupitia mikopo nafuu na mafunzo ya ujasiriamali ili kukuza uchumi na kipato chao. Kadhalika, niwaombe wadau wote wakiwemo vyama vya ushirika, taasisi za kifedha na taasisi za kijamii kuendelea kuiunga mkono Serikali katika jitihada zake za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwawekea mazingira mazuri na rahisi wakati wa kupata huduma zao.

**Uchapishaji na Usambazaji Habari**

**45. Mheshimiwa Spika;** Sekta ya habari ni miongoni mwa sekta iliyochukua kasi katika ulimwengu wa leo. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ya kuimarisha sekta hiyo. Serikali imeongeza uwezo wa uzalishaji wa kazi za uchapaji katika Kiwanda chetu cha Uchapishaji kilichopo Maruhubi kwa kununua mtambo maalum wa kisasa wa uchapishaji unaojulikana kama *Die-Cutting Machine.* Upatikanaji wa mashine hiyo umeongeza ufanisi na kasi ya uzalishaji na ubora wa kazi na kupunguza kwa kiasi kikubwa muda wa upatikanaji wa huduma kwa taasisi za Serikali na sekta binafsi.

**46. Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa sekta ya Utangazaji Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa habari, elimu na burudani kwa jamii kupitia vipindi mbalimbali vya redio na televisheni vinavyolenga kuelimisha, kuburudisha na kuwahabarisha wananchi. Aidha, vituo vya habari vimeendelea kurusha matukio muhimu ya kitaifa na kimataifa ili kuwapa uelewa wananchi juu ya maendeleo ya masuala mbalimbali yanayojiri nchini na duniani kwa jumla. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na vyombo vyote vya habari katika kuhakikisha jamii yetu inapata habari bila kuathiri mila na silka zetu. Serikali itaendelea kusimamia maadili ya vyombo hivyo wakati vinapofanya kazi zake ili kuimarisha maadili ya jamii na kuendeleza utamaduni wa Kizanzibari.

**Maendeleo ya Michezo**

**47. Mheshimiwa Spika;** Serikali imeendeleza sekta ya michezo kupitia ujenzi wa miradi ya kimkakati, ikiwemo Mji wa Michezo wa Fumba wenye uwanja wa kisasa wenye uwezo wa kuchukua watazamaji **36,500.** Uwanja huu unatarajiwa kuwa miongoni mwa viwanja vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vitakavyotumika katika Mashindano ya AFCON 2027. Serikali pia, imekamilisha ukarabati wa viwanja vya Gombani na Mao ze Dong na hivi sasa vinaweza kutumika. Hatua hizi, zinaenda sambamba na ujenzi wa viwanja vya mikoa na wilaya Unguja na Pemba, ambazo zinalenga kukuza vipaji vya vijana na kuongeza fursa za michezo nchini.

**48.Mheshimiwa Spika;** Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa vyama na vilabu vya michezo katika kukuza michezo na kuhakikisha ushiriki wa ushindani kwa vilabu na timu za Zanzibar katika mashindano mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali itaendelea kuratibu mafunzo ya kitaalamu kwa wanamichezo na makocha ili kuongeza kiwango cha utaalamu wao. Nawasihi wanamichezo wenzangu wote nchini kuunga mkono jitihada hizi zinazochukuliwa na Serikali, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kukuza vipaji vya vijana wetu na kuimarisha michezo.

**Uendelezaji Miundombinu na Matumizi ya Masoko**

**49. Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa uendelezaji wa masoko, Serikali imekamilisha ujenzi wa masoko ya kisasa katika maeneo tofauti yakiwemo Kwanyanya, Mombasa, Kitope, Kengeja, na Mzambarauni. Kwa sasa masoko ya Mombasa na Kitope tayari yameanza kutoa huduma, huku masoko ya Kengeja na Mzambarauni yakiwa katika hatua za mwisho za maandalizi ili kuanza kufanya kazi. Masoko haya pamoja na yale ya awali yakiwemo ya Mwanakwerekwe na Jumbi ni mkakati wa kusogeza huduma muhimu kwa wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kurahisisha upatikanaji wa bidhaa na huduma, kupunguza gharama za usafirishaji kwa wafanyabiashara wadogo na kuwa na mazingira mazuri ya kibiashara yatakayowawezesha wananchi kuongeza kipato chao na kuchangia katika Pato la Taifa.

**50. Mheshimiwa Spika;** Napenda kuwasihi na kuhimiza wananchi wote kuyatumia masoko haya kikamilifu ikiwa ni fursa adhimu ya kujikwamua kiuchumi kupitia biashara na ujasiriamali. Aidha, natoa wito kwa mamlaka zinazohusika na jamii kwa jumla kuhakikisha miundombinu hii inatumika kwa uangalifu mkubwa na kuitunza ili iweze kudumu kwa muda mrefu na kuwanufaisha vizazi vya sasa na vijavyo. Ni jukumu la kila mtumiaji kuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya matumizi iliyowekwa na Mamlaka husika ili kuhakikisha masoko yetu yanabaki kuwa maeneo salama, nadhifu na yenye tija kwa maendeleo yetu wenyewe na nchi kwa jumla. Serikali inawatahadharisha wale wote watakaobainika kuharibu au kuhujumu miundombinu ya masoko haya, haitosita kuchukua hatua za kisheria dhidi yao ikiwemo sheria zinazohusu uhujumu wa mali za umma.

**Maendeleo ya Sekta Mtambuka**

**Kuimarisha Utawala Bora**

**51. Mheshimiwa Spika;** katika kukuza ubora wa huduma na kuongeza uwajibikaji, Serikali inahakikisha watumishi wanapata mazingira bora ya utendaji kazi kwa kuwajengea uwezo ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma. Katika kufikia azma hio, mbali na kuimarisha miundombinu kwa kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) Tunguu na Chuo cha IPA Pujini-Pemba, Serikali kupitia Chuo cha Utawala wa Umma, imetoa mafunzo maalum kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Wakuu wa Taasisi kwa lengo la kuimarisha uongozi bora, ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu ya utumishi wa umma.

**52. Mheshimiwa Spika;** Aidha, Serikali imefanya ukaguzi wa hesabu za Serikali kwa njia za kisasa kwa kuzingatia vipaumbele vyake. Ukaguzi huo umefanyika kwa ufanisi mkubwa katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, vituo vya afya, miundombinu ya maji safi na salama, ujenzi wa masoko na vituo vya wajasiriamali.

**53. Mheshimiwa Spika;** Serikali kupitia Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) imefanya ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo **233** Unguja na Pemba yenye wastani wa thamani ya **Shilingi Trilioni 2.29** na Dola za Kimarekani **Milioni 859.42** ili kuona utekelezaji wake kwa kuzingatia ubora wake na thamani ya fedha katika miradi hiyo. Aidha, kwa mwaka wa fedha, 2025/2026 ZAECA imefanikiwa kuokoa kiasi cha Shilingi **5,480,187,032.88** na Dola za Kimarekeni **203,135.84** kati ya hizo **Shilingi 4,233,659,348.88** na **Dola 201,035.84** zilirudishwa Serikalini na **Shilingi 1,246,527,684.00** na **Dola 2,100** zilirudishwa kwa wananchi.

**54. Mheshimiwa Spika;** napenda kuwasisitiza viongozi na watumishi kuzingatia na kuyatumia ipasavyo mafunzo yanayotolewa juu ya utumishi wa umma ili kujiimarisha katika utoaji wa huduma, usimamizi wa miradi na rasilimali za umma pamoja na kuhakikisha kuwa wanaleta mabadiliko chanya kwa wananchi na serikali kwa ujumla. Hii itaongeza na kujenga imani zaidi ya wananchi juu ya huduma bora zinazotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

**55. Mheshimiwa Spika;** Serikali kwa upekee mkubwa inaendelea kulichukulia suala la mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa umuhimu mkubwa ili kukiokoa kizazi cha leo na kesho katika mateso na idhilali zinazotokana na matumizi ya dawa hizo. Aidha, kupitia Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Serikali imemkamata raia mmoja wa Romania na wenzake kwa kuingiza dawa za kulevya na kuyachanganya kwenye vyakula vya kawaida. Vyakula hivyo ni pamoja na Pipi, Korosho na Biskuti ambapo huchanganywa na dawa za kulevya na kuyauza kwenye *Supermarkets* na Maduka mengine ya kawaida. Hali hii hupelekea athari hata kwa watoto ambao baadae wanaweza kuwa waraibu kwa kuzoea kutumia dawa za kulevya bila ya kukusudia.

**56. Mheshimiwa Spika;** katika kupambana na kadhia hiyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhitibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeyafunga maduka hayo, pamoja na ghala moja (1) lililopo Mpendae ambalo ndilo linalotumiwa kwa kuchanganyia dawa hizo kwenye vyakula vilivyotajwa hapo awali na kesi ya watuhumiwa hao inaendelea. Aidha, Serikali imefungua kesi **48** (Unguja **40** na Pemba **8**) ambapo watuhumiwa **53** (wanaume **45**, wanawake **8)** walikamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya aina ya bangi, mirungi, heroini na kokeni.

**57. Mheshimiwa Spika;** Mapambano dhidi ya uingizaji, usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya yameimarika ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kilogramu **1,525.3** za dawa za kulevya zilikamatwa. Vilevile, Serikali imetaifisha mali ikiwemo nyumba, gari, mashamba na nyenginezo zenye thamani ya **Shilingi 1,135,800,000** ikilinganishwa na **kilogramu 1,449** za dawa za kulevya zilizokamatwa pamoja na kutaifisha mali zenye thamani ya **Shilingi 976,052,016** kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mafanikio haya yamepatikana kutokana na ongezeko la operesheni, utoaji wa maamuzi ya kesi za uhalifu wa dawa za kulevya na utaifishaji, kuimarika kwa mbinu za ukamataji pamoja na ushirikiano unaopatikana kutoka kwa wananchi.

**58. Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa uimarishaji wa miundombinu ya kurekebisha tabia, Serikali imekamilisha hatua za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa kituo cha wanawake cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kangagani- Pemba. Kituo hicho kitasadia waathirika wa dawa za kulevya kupata huduma muhimu za kuwapatia Tiba na huduma nyingine kwa upande wa Pemba. Sambamba na hilo, Serikali imeanzisha Kituo cha mawasiliano ya dharura kwa kurahisisha utoaji wa taarifa kutoka kwa wananchi kuhusu

uhalifu wa dawa za kulevya. Lengo ni kuiwezesha jamii kutoa taarifa za matukio au viashiria vya uhalifu wa dawa za kulevya wakati wowote, kwa haraka na usiri kwa kutumia namba ya bure **119.**

**59. Mheshimiwa Spika;** niwahakikishie wananchi wenzangu kuwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea na mapambano dhidi ya dawa za kulevya, ikiwemo ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kiuchunguzi na udhibiti wa bandari bubu pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma za Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha mashirikiano na wananchi pamoja na kuwajengea uwezo na mbinu maafisa wa doria katika kutoa taarifa za wahalifu wa dawa za kulevya.

**60. Mheshimiwa Spika;** ninawanasihi wananchi wote tuendelee kushirikiana kwa hali zote katika kupambana na dawa za kulevya ili kukikinga kizazi chetu cha sasa na kijacho na madhara yanayotokana na utumiaji wa dawa hizo. Madhara ya matumizi ya dawa hizo hayamuathiri mtuamiaji peke yake bali jamii pia ikiwemo kukosekana kwa nguvu kazi na kushuka kwa uchumi wa familia na nchi kwa jumla.

**Haki na Fursa kwa Watu wenye Ulemavu**

**61. Mheshimiwa Spika;** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi imeendelea na utoajii wa haki na fursa kwa Watu wenye Ulemavu. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imewapatia jumla ya vifaa saidizi **773** vikiwemo Motor Wheelchair 60, Sun screen lotion kwa watu wenye ulemavu wa ngozi **377**, kofia **236** na miwani **100** vyenye thamani ya **Shilingi 894,950,000** ikilinganishwa na vifaa saidizi **425** vyenye thamani ya **Shilingi 325,500,000** vilivyotolewa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**62. Mheshimiwa Spika;** Serikali kupitia Baraza la Watu wenye Ulemavu pamoja na kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeendelea kuimarisha uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa kuboresha mfumo wa utoaji mikopo. Serikali imetoa unafuu wa masharti ya mikopo kupitia **programu ya 4:4:2** ambapo kwa hivi sasa tumepunguza masharti yaliyokuwepo hapo awali yaliyotaka mikopo wapewe vikundi tu. Hivi sasa sharti hilo limeondolewa na Mamlaka inatoa fursa kwa mjasiriamali mmoja mmoja mwenye Ulemavu  kuweza kupata mikopo hiyo. Hatua inayolenga kuongeza tija na uhuru wa usimamizi wa miradi na kujitegemea.

**63. Mheshimiwa Spika;** Pamoja na hayo, Serikali imefanya ongezeko la bajeti ya uwezeshaji, ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya **Shilingi 79,780,000** zimetolewa kwa walengwa hao, ikiwa ni ukuaji wa takriban **asilimia 85** ikilinganishwa na **Shilingi 43,200,000** zilizotolewa katika kipindi cha mwaka 2024/2025. Jitihada hizi ni kielelezo cha dhamira ya Serikali ya kutoa kipaumbele katika kukuza kipato na ustawi wa Watu wenye Ulemavu nchini. Hadi kufikia Machi 2026 jumla ya vikundi viwili (**2**) vinavyojumuisha wanufaika **37** (wanaume **18** na wanawake **19**) na mtu mmoja mmoja **29** (wanaume **21** na wanawake **8**) wamepatiwa mikopo hiyo.

**64. Mheshimiwa Spika;** Serikali itaendeleza dhamira yake ya dhati ya kukuza ustawi wa Watu wenye Ulemavu kupitia mikakati jumuishi. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha miundombinu rafiki, kutoa elimu bora, upatikanaji wa huduma za afya, fursa za michezo, na ajira zenye staha. Natoa wito kwa Watu wenye Ulemavu nchini kuendelea kuzichangamkia fursa hizi za mikopo na mafunzo zinazotolewa na Serikali na wadau wengine ili kujiimarisha kiuchumi na kijamii kwa manufaa na maendeleo yao na nchi kwa jumla.

**Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira**

**65. Mheshimiwa Spika;** Serikali imeendelea kuchukua juhudi za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kukamilisha mikakati ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo NDCs na NAP. Aidha, imefanya tathmini ya maeneo **60** yanayoingia maji ya chumvi na matayarisho ya michoro na gharama za ujenzi wa matuta, kuta za kuzuia maji ya chumvi pamoja na programu mbili (**2**) za kuinua kipato cha wananchi katika maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi. Vile vile, Serikali imekamilisha matayarisho ya Mradi wa jamii ikiwemo mchoro (board walk) na gharama za ujenzi wa eneo la mikoko liliopo Tibirinzi Pemba kwa ajili ya kuvutia watalii.

**66. Mheshimiwa Spika;** jitihada mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa katika kuimarisha usimamizi wa mazingira ikiwemo kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kilogramu **2,263** (Unguja kilogramu **1,736.5** na Pemba kilogramu **526.5**) zimekamatwa na kutozwa faini ya **Shilingi 9,100,000** (**7,990,000** Unguja na **1,110,000** Pemba) ikilinganishwa na **kilogramu 400** zilizokamatwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Haya ni mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki kupitia operesheni **54** katika maghala makubwa yanayohifadhi bidhaa mbali mbali Unguja na Pemba.

**67. Mheshimiwa Spika;** napenda kuwahamasisha wadau, mamlaka za utekelezaji na jamii kwa ujumla kuendeleza ujenzi wa miundombinu na utekelezaji wa miradi ya kuinua kipato katika maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi Unguja na Pemba. Sambamba na kuongeza kasi ya ushiriki wa pamoja katika kutekeleza Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani ili kuhakikisha uhifadhi endelevu wa mazingira yetu.

**Kuimarisha na Kuendeleza Amani na Utulivu**

**68. Mheshimiwa Spika;** amani na utulivu ndio msingi mkuu wa maendeleo ya taifa letu, kwani bila amani na utulivu hakuna mipango ya kiuchumi wala miradi ya kijamii inayoweza kutekekelezeka. Itakumbukwa kuwa tayari tumemaliza kipindi cha uchaguzi kwa mwaka 2025, ni vyema sote tukatambua kuwa amani tuliyonayo ni dhamana tunayotakiwa kuilinda kwa nguvu zetu zote, kwani amani na utulivu ni mazingira pekee yanayomruhusu kila mwananchi kutekeleza majukumu yake bila hofu.

**69. Mheshimiwa Spika;** utulivu tulionao katika nchi yetu unadhihirisha ukomavu wetu katika kuthamini amani tuliyonayo, hivyo tuendelee kuweka kando tofauti zetu za kisiasa na sote tuelekeze nguvu zetu katika kujenga nchi yetu kwa ajili ya ustawi wa sasa na vizazi vijavyo. Nawaomba sana wananchi wenzangu tuendelee kuungana katika kusimamia amani na utulivu kwa moyo mmoja tukiwa na dhamira ya kuiletea nchi yetu maendeleo. Kila mmoja wetu aichukulie amani kuwa ni jukumu letu la msingi na si la vyombo vya ulinzi pekee kwa kuepuka chuki na uchochezi pamoja na kuvumiliana katika tofauti zetu na kuwa walinzi wa nchi yetu.

**70. Mheshimiwa Spika;** maelezo niliyoyawasilisha ni muhtasari wa mafanikio na mikakati katika masuala mbalimbali ya kisekta, ambapo ufafanuzi wa kina, uchambuzi wa utekelezaji, na ukamilifu wa taarifa hizi utatolewa na Waheshimiwa Mawaziri wa sekta husika wakati watakapowasilisha hotuba za makadirio ya bajeti ya Wizara zao.

**71. Mheshimiwa Spika;** sasa kwa ridhaa yako naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 na malengo ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

## UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI 2025/2026)

**72. Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inatekeleza kazi za kawaida na miradi ya maendeleo kupitia Idara saba na Taasisi tatu ambapo kwa kutumia Bajeti inayotumia Programu (Programme Based Budget) kazi hizo zinatekelezwa kupitia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14. Aidha, kupitia Programu hizo, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi imetekeleza kazi zake chini ya Mafungu Matatu ya kibajeti ambayo ni:

i C01 – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

ii C02 – Baraza la Wawakilishi, na

iii C03 – Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

**73. Mheshimiwa Spika;** katika kipindi cha Julai – Machi 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Program zake imetekeleza kazi za kawaida kama ifuatavyo:

### C01 – OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

**PROGRAMU KUU - C0101: URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

**Programu Ndogo - (SC010101): Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais**

**74. Mheshimiwa Spika;** Programu hii ina Programu Ndogo moja ya Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais ambayo ina jukumu la kuratibu kazi za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais pamoja na utoaji wa huduma zote muhimu anazostahiki Makamu wa Pili wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo: -

i. Imeratibu ziara za ndani 21 za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar zilizolenga kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali na maendeleo kwa wananchi katika maeneo yao;

ii. Imeratibu Mikutano/Vikao 14 rasmi vya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na wageni mbali mbali wakiwemo viongozi na watendaji wa Serikali, Wawekezaji na Wageni Mashuhuri wa ndani na nje ya nchi;

iii. Ofisi imepokea na kuratibu ufumbuzi wa malalamiko/migogoro 54 baina ya pande tofauti ambapo migogoro minne **(04)** imepatiwa ufumbuzi na migogoro 50 imesikilizwa na kuwasilishwa katika Taasisi na Wizara husika. Ofisi inaendelea kufuatilia hatua zinazochukuliwa katika kuyapatia ufumbuzi malalamiko yaliyobakia yaliyopo katika Wizara/Taasisi mbali mbali za Serikali;

iv. Ofisi imeendelea kutoa taarifa juu ya shughuli na matukio **48** aliyofanya/kushiriki Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, imehifadhi kumbukumbu za hotuba **41** na picha **420** zinazohusiana na kazi za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kumbukumbu na matumizi ya mengine.

v. Imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo aliyotoa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa wananchi, taasisi na jamii yanayolenga kutatua changamoto na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wahusika;

**75. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii inayotekelezwa na Afisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,023,250,000** kazi za kawaida ambapo **Shilingi 1,347,981,000** ni za mshahara na **Shilingi 675,269,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2026 Ofisi kupitia Programu hii imetumia **Shilingi 1,166,166,155** ambazo ni sawa na **asilimia 75** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 58** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

## PROGRAMU KUU - (C0102): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

**76. Mheshimiwa Spika;** Jukumu la Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ni kuweka mfumo imara na endelevu wa utoaji na upatikanaji wa huduma bora za Serikali kwa jamii. Programu hii ina Programu Ndogo nne ambazo ni Kukabiliana na Maafa, Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shughuli za SMZ – Dodoma. Maelezo ya utekelezaji wa kazi kwa kila Programu Ndogo ni kama ifuatavyo:

## Programu Ndogo – (SC010201): Kukabiliana na Maafa

**77. Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina jukumu la kuratibu masuala yote ya kukabiliana na maafa hapa Zanzibar kwa kuratibu na kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Kukabiliana na Maafa ambayo inalenga kujenga uhimili wa jamii katika kujikinga na kukabiliana na maafa katika maeneo yao. Katika kipindi cha Julai – Machi cha mwaka wa fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa ilitekeleza yafuatayo: -

i. Imetoa elimu ya kujikinga, kujiandaa na kukabiliana na maafa kwa makundi mbalimbali ya jamii wakiwemo wanafunzi **5,666** wa Skuli za Msingi na Sekondari (Wanaume **2,039** na Wanawake 3**,627**), watumishi **45** (wanawake 25 na wanaume 20) wa Baraza la Mji Kusini Unguja na waendesha Bajaji na Boda boda **100** na wananchi **150** kwa Wilaya za Kaskazini "A" na Mjini Unguja, Wenyeviti wa Kamati za Kukabiliana na Maafa za shehia za Wilaya ya Kati, Kamati ya Kitaalam ya Kukabiliana na Maafa ya Wilaya ya Kati, pamoja na Madiwani Wilaya ya Magharibi "A" Unguja, Wajumbe 16**0** (wanawake **82** na wanaume **78)** wa Kamati za Kukabiliana na Maafa za Shehia **14** za Wilaya za Kaskazini A, Magharibi A na Mjini. Elimu hiyo imetolewa kwa mashirikiano na Taasisi mbalimbali zikiwemo Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Jeshi la Polisi kutegemea na aina ya mafunzo na maudhui yaliyokusudiwa;

ii. Elimu ya kukabiliana na maafa vilevile imetolewa kupitia vyombo vya habari ambapo jumla ya vipindi **20** pamoja na matangazo **25** yamerushwa hewani kupitia ZBC TV na Redio, Zanzibar Cable, Bahari FM, Zenji FM na Asam TV online pamoja na mitandao ya kijamii;

iii. Imetoa taarifa za tahadhari za mapema juu ya muelekeo wa mvua za Vuli za mwaka 2025 na mvua za Masika za mwaka 2026 na athari zinazoweza kujitokeza kwa jamii na kwa wadau maalum kulingana na majukumu na maeneo yao ya kazi. Miongoni mwa wadau hao ni Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za Kukabiliana na Maafa za Wilaya, Walimu Wakuu wa Skuli za Wilaya ya Chake Chake na Taasisi **41** za Serikali na Binafsi. Vilevile, tahadhari zimetolewa juu ya uwezekano wa kuwepo kwa upepo mkali na mafuriko kupitia matangazo ya redio na televisheni na ujumbe mfupi wa pamoja (bulk

SMS) kwa Kamati za Uvuvi na Masheha ili kuchukua hatua stahiki katika kujikinga na majanga hayo na mengine yanayoweza kutokea;

iv. Tahadhari za mapema pia zimetolewa kwa makundi saba (**7**) yaliyo katika mazingira hatarishi ya kuathiriwa na maafa Unguja na Pemba yakiwemo watu wenye mahitaji maalum, wavuvi, wanawake, vijana, wazee, wafugaji na wakulima, waendesha bodaboda na bajaji na watu wanaoishi maeneo hatarishi;

v. Ofisi imeratibu operesheni na utoaji wa huduma za misaada ya kibinaadamu katika matukio **447** ya majanga yaliyotokea Unguja na Pemba. Kati ya hayo, matukio **233** ni ya moto, matukio 10 ya upepo mkali, **11** ya kuzama baharini, ajali za barabarani matukio 184 na matukio matano (**5**) ya mafuriko. Matukio hayo yamepelekea vifo vya watu **207** na majeruhi **98**. Kufuatia matukio hayo, Ofisi imeratibu na kutoa misaada ya kibinaadamu ikiwemo kuwapatia magodoro, blanketi, vyandarua, nguo, sare za skuli na mabuku kwa wanafunzi pamoja na kutoa mkono wa pole kwa ndugu na jamaa waliofiwa na jamaa zao na huduma za matibabu kwa waliojeruhiwa kutokana na majanga/maafa yaliyotokea;

vi. Ofisi imeratibu na kushiriki katika kaguzi **16** katika taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Kiserikali ili kubaini mipango yao pamoja na uzingatiaji wa miongozo na taratibu za kukabiliana na maafa katika maeneo yao. Miongoni mwa maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi ni Kiwanja kipya cha mpira kinachojengwa Fumba, Bandari ya Mkokotoni, Bandari ya Malindi na Bandari ya Maruhubi, Hoteli za Verde, Cave Paje, Skuli ya Msingi na Sekondari Mtumwajeni. Baada ya ukaguzi huo Ofisi kupitia Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa ilichukua hatua stahiki zikiwemo kutoa maelekezo kwa wahusika juu ya kufuata miongozo ya kukabiliana na maafa katika maeneo yao kama vile kuwa na mipango ya uokozi (evacuation plan) na maeneo ya kufikia wakati wa dharura (assembling point). Aidha, ilisitisha shughuli za masomo kwa muda katika Skuli ya Msingi na Sekondari Mtumwajeni kwa kukosa viwango na kuwa katika mazingira hatarishi yanayoweza kusababisha maafa;

vii. Ofisi imeziimarisha ghala za kuhifandhia vifaa vya operesheni na misaada ya kibinadamu kwa kuzifanyia matengenezo pamoja na kununua vifaa mbali mbali vikiwemo mabati 360, magodoro 30, Kanga mivao 20, pea 100 za viatu (rainboat) na barakoa boksi 80 ambazo zitatumika wakati wa dharura kama itakavyoelekezwa;

viii. Ofisi iliratibu Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupunguza Athari za Maafa Duniani ambapo shuhguli mbalimbali zilifanyika zikiwemo midahalo ya wanavyuo, makongamano na kilele cha maadhimisho hayo. Kilele cha maadhimisho hayo kilifanyika katika Kituo cha Mabasi kilichopo soko la Chuini ambapo jumla ya wanajamii 1,457 walipatiwa huduma za afya na waliogundulika kuwa na changamoto za kiafya walipatiwa matibabu, ushauri na rufaa katika hospitali husika ili waendelee kuwa na afya bora;

ix. Imeratibu na kuhudhuria vikao mbalimbali vya kiutendaji vikiwemo vikao vya pamoja vya Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Manispaa na Mabaraza ya Miji ya Wilaya za Kaskazini A, Kaskazini B, Mjini na Magharibi B Unguja, kwa ajili ya kuwakumbusha haja ya kuitishwa kwa vikao vya Kamati za Kukabiliana na Maafa za Wilaya zao, kikao kimoja kilichojadili haja ya kuandaa Mpango Mkuu wa Utiririshaji na Uvunaji wa Maji ya Mvua (Storm Water Management Master Plan) kwa lengo la kupunguza athari za mvua kubwa ndani ya Zanzibar kufuatia ripoti ya tathmini ya kutuama kwa maji ya mvua na utiririshaji wa maji taka katika pwani ya Mkoa wa Mjini Magharibi na kikao cha Afya Moja kilichowashirikisha wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi na wataalamu kutoka Taasisi mbali mbali hapa Zanzibar pamoja na kuwapatia mafunzo wataalamu 35 wa Taasisi mbali mbali zinazoshughulika na masuala ya Afya Moja kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuweka mikakati ya kudhibiti maradhi yanayotokana kwa wanyama kwenda kwa binadamu yakiwemo, Homa ya Nyani, Ebola na Mulburg;

**78. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,176,000,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2026 imetumia **Shilingi 1,288,507,323** ambazo ni sawa na **asilimia 77** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 59** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

## Programu Ndogo – (SC010202): Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa

**79. Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa inatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 – Machi 2026)

Programu hii Ndogo imetekeleza yafuatayo: -

i. Imeratibu Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambazo zimejumuisha ukaguzi wa miradi ya maendeleo pamoja kushiriki katika Sherehe za ufunguzi na uwekaji wa mawe ya msingi. Jumla ya miradi yote iliyohusika ni 110 ambapo miradi 64 ilizinduliwa/kufunguliwa na miradi 46 iliwekewa mawe ya msingi Unguja na Pemba.

ii. Imeshiriki katika uratibu wa sherehe ya kumuapisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi zilizofanyika katika Uwanja wa Amaan Complex pamoja na kushiriki katika sherehe za kumuapisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan zilizofanyika Chamwino Dodoma;

iii. Imeshiriki katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa yaliyofanyika tarehe 25, Julai 2025 jijini Dodoma ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan;

iv. Imeshiriki katika vikao vya awali vya maandalizi ya maadhimisho ya Miaka 62 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambazo kilele chake huwa tarehe 26 Aprili, ya kila mwaka;

v. Imeratibu maandalizi ya Maadhimisho ya Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa na Siku ya Kumbukumbu ya Sheikh Abeid Amani Karume ambayo yalianza tarehe 1 Aprili, 2026 na kukamilika tarehe 7 Aprili, 2026. Maandalizi yalihusisha vikao vitatu vya Kamati, ziara za ukaguzi katika maeneo yatakayosomwa dua na kuratibu marekebisho katika maeneo ya yatakayofanyika shughuli mbalimbali;

vi. Imeratibu na kushiriki katika maonesho ya Kumbukizi ya Baba wa Taifa na Wiki ya Vijana kwa kuandaa banda la Kumbukumbu ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume yaliyofanyika Mbeya kuanzia tarehe 7 Oktoba, 2025 na kuhitimishwa tarehe 14 Oktoba, 2025 wakati wa kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa;

vii. Imeendelea kutoa huduma za ukodishaji wa vifaa vya sherehe pamoja na ukodishaji wa maduka yaliyopo Mwanakwerekwe.

**80. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,018,792,000** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 321,791,000** za mshahara na **Shilingi 1,697,001,000** ni za matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2026 fedha zilizopatikana ni **Shilingi 1,962,021,530** ambazo ni sawa na **asilimia 103** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 97** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

**81. Mheshimiwa Spika;** Programu hii Ndogo vilevile, inahusika na ukusanyaji wa mapato kutokana na ukodishaji wa vifaa vya sherehe na maduka yaliyopo Mwanakwerekwe. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026, Programu hii Ndogo ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 27,240,000** na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2026 kiasi kilichokusanywa ni **Shilingi 19,975,000** ambayo ni sawa na **asilimia 82.8** kwa fedha iliyotengwa miezi tisa na **asilimia 73.3** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

## Programu Ndogo – (SCO10203): Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

**82. Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina jukumu la kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na masuala ya Muungano, kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, Utafiti kitaifa pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) hapa Zanzibar. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali na katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 – Machi 2026), imetekeleza yafuatayo:

i. Imepanga na kubainisha Ibara za Maagizo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025 kwa kila Wizara na kuweka katika mfumo wa Uratibu wa Shughuli za Serikali pamoja na kuandaa taarifa ya SMZ kuhusu utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2025 kwa kipindi cha siku 100 za Serikali ya Awamu ya Nane na Kipindi cha Pili kuingia Madarakani;

ii. Imeandaa Rasimu ya Mwelekeo wa Miaka Mitano ya Utekelezaji wa Shughuli za Serikali kwa ngazi ya Mikoa ya Zanzibar;

iii. Imeweka hewani Mfumo wa Uratibu wa Shughuli za Serikali (Dashbodi) ambao unapatikana kupitia tovuti ya www.utekelezaji.ompr.go.tz. Aidha, Ofisi iliandaa vikao mbali mbali vya maboresho ya Mfumo huo na kuunganisha

na mifumo mingine ili kurahisisha upatikanaji na usambazaji wa taarifa husika. Miongoni mwa vikao hivyo ni baina ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na e-GAZ, ZPDB na Tume ya Mipango Zanzibar na Kamati ya Makatibu Wakuu wa SMZ. Mfumo huu tayari umeunganishwa na Mfumo wa ZiPS ambao umewezesha miradi ya kimkakati na ya kawaida kuonekana katika mfumo;

iv. Imeandaa kitabu cha Utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa kipindi cha miaka minne (2020 – 2024) ambacho ni rejea muhimu kwa watunga sera, watafiti na wanasiasa. Ofisi vilevile imeratibu na kuandaa vikao kazi vya tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

v. Imetoa mafunzo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wakurugenzi na Maafisa Mipango wa Serikali za Mitaa na Wajumbe wa Kamati za Mfuko huo Unguja na Pemba;

vi. Imeandaa Moduli ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ili kuwezesha shughuli za Mfuko kufanyika kwa njia ya kidigitali. Kazi hiyo imefanywa kwa ushirikiano wa Wataalamu kutoka Tume ya Mipango Zanzibar katika Mfumo wa ZiPS;

vii. Ofisi iliandaa kikao cha Wakurugenzi na Maafisa Mipango wa Serikali za Mitaa Unguja na Pemba ili kukusanya maoni na ushauri kwa ajili ya kuboresha Moduli ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF);

viii. Imeratibu na kuandaa ziara maalum ya Shirika la Utangazaji la Manhwa (MBC) la Jamhuri ya Korea kupitia Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA) ambayo ilikagua baadhi ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na KOICA kupitia Sekta ya Uchumi wa Buluu na Elimu na kuandaa Makala Maalum ya Utalii;

ix. Imeratibu na kusimamia upatikanaji wa vibali vya utafiti ambapo jumla ya vibali 941 vilitolewa kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi ikijumuisha Taasisi 36 (Taasisi 11 za Serikali na Taasisi 25 za Binafsi), wageni walikuwa ni 55 na Wenyeji ni 850. Aidha, vibali 473 vilitolewa kwa wanawake na 429 kwa wanaume kutoka katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi;

x. Imeendelea na taratibu za kuandaa mfumo wa maombi ya vibali vya utafiti ambapo jumla ya vikao vitano vya majadiliano vilifanyika. Vikao hivyo

vilihusisha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Tume ya Kitaifa Sayansi na Teknolojia (COSTECH); OCGS na e-GAZ; Taasisi ya Utafiti wa Afya (ZAHRI), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo (ZALIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Rasilimali za Bahari; na Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji Zanzibar;

xi. Imeratibu na kuandaa vikao vya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Lishe ambavyo vilihusisha kamati ya wataalamu (Technical Working Group – TWG na Kamati ya Usimamizi ya Kisekta (Inter - Sectorial Management Committee – IMC). Vikao hivyo viliandaa Hadidu Rejea za Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe wa mwaka 2024/2025-2028/2029 (ZMNSAP); kupitia maeneo makuu ya utekelezaji wa Mkakati; kutoa uelewa kwa Wakurugenzi juu ya ZMNSAP na kutoa maelekezo juu ya maandalizi ya Kikao cha Kamati Tendaji ya ZMNSAP.

xii. Iliandaa Kikao cha Kamati ya Wataalamu ya Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Lishe Zanzibar ambacho kilipokea matokeo ya Utafiti wa Tathmini wa Gharama za Lishe Zanzibar. Aidha kikao kilijadiliana kuhusu maeneo ya utekelezaji wa Afua za Lishe kupitia Wizara zote zinazoguswa na maeneo ya utekelezaji;

xiii. Iliratibu na kushiriki kuandaa kitabu cha utafiti wa gharama za utapiamlo ya Zanzibar na Tanzania Bara (COHA) kwa kushirikiana na Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ripoti ya Utafiti huo inabainisha kuwa, mwaka 2022, Zanzibar ilipata hasara za kijamii na kiuchumi zinazokadiriwa kufikia **Shilingi Bilioni 354.5 (USD milioni 153.1)** kutokana na utapiamlo wa watoto;

xiv. Iliratibu na kuandaa kikao kazi cha sekta Mtambuka cha mapambano dhidi ya Malaria kwa Makatibu Wakuu wa SMZ ambacho kilielekeza Wizara zote za SMZ zishirikishwe kutoa` maoni katika maeneo yaliyoandaliwa kutekelezwa ili Zanzibar itokomeze Malaria kabla ya mwaka 2030;

xv. Iliratibu na kuandaa kikao kilichojadili lalamiko la kusitishwa kwa utekelezaji wa mradi uliowezeshwa na COSTECH ambao kwa sasa umeanza upya kutekelezwa chini ya usimamizi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar (ZALIRI);

xvi. Ofisi imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majimbo 32 ya Unguja. Pia, imeratibu na kushiriki katika Semina kuhusu Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo na Majukumu ya Taasisi za Muungano kwa Wabunge na Wakurugenzi wa Serikali za mitaa kutoka Zanzibar;

xvii. Imeziratibu sekta za SMZ pamoja na kushiriki warsha ya kukuza uelewa kuhusu Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai (NBSAP 2025-2030) nje ya maeneo ya hifadhi;

xviii. Ofisi iliratibu na kushiriki katika semina kuhusu Muungano kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Aidha, iliandaa semina kwa Wahariri wa vyombo vya habari kuhusu elimu ya Muungano ambayo ilishirikisha Wahariri na Waandishi wa Vyombo vya Habari 40. Vilevile, iliratibu na kushiriki katika Kongamano kuhusu Elimu ya Muungano na jinsi ya kulinda na kudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa wanafunzi wa vyuo vya Elimu ya juu Zanzibar.

xix. Imefuatilia utekelezaji wa miradi sita (6) ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Polisi Zanzibar. Miradi mitano (5) ni ya Idara ya Uhamiaji na mmoja (1) ni wa Jeshi la Polisi;

xx. Imeandaa na kushiriki katika kikao cha kupitia Rasimu ya Taarifa ya Utekelezaji wa hoja za Muungano zilizopatiwa Ufumbuzi;

xxi. Imeratibu na kushiriki vikao vitano (5) vya mashirikiano baina ya Wizara/ Sekta za SMZ na SJMT vifuatavyo:

a. Wizara ya Uchukuzi (SJMT) na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (SMZ) katika Sekta za Uchukuzi kilichofanyika katika Ukumbi wa Maji House, Zanzibar;

b. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) na Ofisi ya Makamu wa Rais (SJMT) ngazi ya Makatibu wakuu pamoja na Ngazi ya Mawaziri kilichofanyika Ukumbi wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Maisara Zanzibar, na

c. Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar (COSOZA) na Afisi ya Hakimiliki ya Tanzania Bara (COSOTA) kilichofanyika katika Ukumbi wa Ofisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar.

xxii. Iliandaa kikao baina ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar, kwa ajili ya kupitia Rasimu ya Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar ambapo jumla ya Taasisi 23 za Muungano zilishiriki;

xxiii. Imeratibu na kushiriki katika kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa na Kumbukizi ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Wiki ya Vijana iliyofanyika Mkoani Mbeya. Pia Ofisi ilisimamia uendeshaji wa Banda Maalumu la Kumbukizi ya Marehemu Sheikh Abeid Aman Karume katika tukio hilo;

xxiv. Imekamilisha uandaaji wa Tathmini ya Hali ya Siasa ya Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano (2020-2025) na kuandaa Kitabu cha Chaguzi mbalimbali na Hali ya Kisiasa Zanzibar kuanzia mwaka 1957 hadi 2025;

xxv. Ofisi imeshiriki katika mikutano ya vyama vyote vya Siasa vilivyosimamisha mgombea wa Urais kwa tiketi ya vyama vyao katika Uchaguzi Mkuu wa 2025 kwa lengo la kuhakikisha uwajibikaji, uwazi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera na ahadi zinazotolewa kwa wananchi katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu;

xxvi. Imefanya uzinduzi wa Mkakati wa Kitaifa wa Vijana wa Kudumisha Amani na Maendeleo Endelevu Zanzibar. Vilevile, kwa kushirikiana na UNDP, Ofisi imeratibu utiaji saini wa Hati ya Makubaliano ya Utoaji wa Mafunzo ya Amali ya Nadharia na Vitendo katika Mradi wa Dumisha Amani II Zanzibar baina ya mamlaka ya Vyuo vya Amali (VTA) na Kampuni ya CRJE. Fani zitakazohusika ni Fundi Bomba, Umeme na Useremala;

xxvii. Ofisi iliratibu mafunzo juu ya Mkakati wa Kitaifa wa Amali yalitolewa kwa ushirikiano na Taasisi isio ya kiserikali ya Center for Youth Dialogue (CYD) kwa vijana 60 (30 Unguja na 30 Pemba) ambapo mafunzo ya nadharia yalitolewa katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Mwanakwerekwe na katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji. Aidha, mafunzo ya vitendo yalifanyika katika Bandari ya Fumba na Hoteli ya Katalunya iliyopo Pwani Mchangani kwa Unguja na katika Bandari ya Mkoani Pemba;

xxviii. Ofisi imeratibu vikao vya utekelezaji wa mradi wa Dumisha Amani II vilivyoandaliwa kwa ushirikiano na UNDP;

xxix. Ofisi imeshiriki na kufuatilia Mkutano wa Kwanza na Pili wa Baraza la 11 la Wawakilishi iliyohusisha shughuli mbalimbali ikiwemo uzinduzi rasmi

uliofanywa na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

xxx. Imeendelea kusimamia shughuli za Idara ya Uhamiaji Zanzibar.

**83. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,657,883,300** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2026 imetumia **Shilingi 3,711,069,353** ambazo ni sawa na **asilimia 86** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 80** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

**84. Mheshimiwa Spika;** vilevile, Baraza hili liliidhinisha matumizi ya **Shilingi 25,573,700,000** ikiwa ni ruzuku kwa Idara ya Uhamiaji, Zanzibar na hadi Machi 2026 ilipata **Shilingi 21,310,000,000** ambazo ni sawa na **asilimia 111** kwa fedha iliyopangwa miezi tisa na **asilimia 83** kwa fedha zilizopangwa kwa mwaka.

**85. Mheshimiwa Spika;** Programu hii Ndogo kupitia Programu ya TASAF pia ilipangiwa **Shilingi 35,100,000,000** kwa kazi za maendeleo ambapo **Shilingi 35,000,000,000** ni mchango wa Washirika wa Maendeleo na **Shilingi 100,000,000** ni mchango wa Serikali. Hadi kufikia Machi 2026 ilipata jumla ya **Shilingi 2,215,514,254** ambazo ni sawa na **asilimia 6** ambapo **Shilingi 2,140,514,254** ni mchango wa Washirika wa Maendeleo sawa na **asilimia 6.2** na **Shilingi 75,000,000** ni mchango wa Serikali sawa na **asilimia 100** kwa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa na **asilimia 75** kwa fedha zilizopangwa kwa mwaka.

## Programu Ndogo – (SCO10204): Shughuli za SMZ – Dodoma

**86. Mheshimiwa Spika;** jukumu kuu la Programu Ndogo ya Shughuli za SMZ, Dodoma ni kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Tanzania Bara kwa lengo la kurahisisha mipango na utekelezaji wa shughuli za SMZ huko Tanzania Bara. Aidha, Programu Ndogo hii inahusika na kukuza na kuimarisha ushirikiano baina SMZ na Serikali na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Kimataifa na Ofisi za Kibalozi zilizopo Tanzania Bara. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii imetekeleza yafuatayo: -

i. Imeratibu na kushiriki vikao 40 vya mashirikiano ya kazi baina ya Wizara za SMZ, SJMT, Ofisi za Kibalozi, Taasisi na Jumuiya za Kimataifa;

ii. Imeratibu na kutoa huduma ya usafiri kwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanapofanya ziara na kuhudhuria mikutano Dar es Salaam na Mikoa mingine Tanzania Bara pamoja na kuratibu upatikanaji VISA tano (5) kwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanawaotarajia kusafiri nje ya nchi;

iii. Ofisi imewapatia mafunzo ya masuala mtambuka kwa Wafanyakazi wa Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma juu ya Afya ya Akili;

**87. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dodoma iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,299,042,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2026 imetumia **Shilingi 566,883,336** ambazo ni sawa na **asilimia 56** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 44** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

## PROGRAMU KUU – CO104: UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

**88. Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu hii ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inahusika na uimarishaji wa mazingira bora ya wafanyakazi na uratibu na simamizi wa mipango, miradi ya maendeleo na shughuli za kiofisi kwa jumla. Programu hii ina Programu Ndogo tatu (**3**) ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu Pemba.

### Programu Ndogo – (CO10401): Uongozi na Utawala

**89. Mheshimiwa Spika;** Programu hii Ndogo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na inahusika na usimamizi wa rasilimali za ofisi na utekelezaji wa kazi za kila siku za Ofisi. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo hii imetekeleza yafuatayo: -

i. Imesimamia maslahi na stahiki za wafanyakazi wa Ofisi zikiwemo za mishahara, likizo, posho, kupandisha madaraja, michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na Mfuko wa Bima ya Afya (ZHSF), pamoja na mafao ya aina tofauti kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi;

ii. Imeendelea kusimamia shughuli za uendeshaji wa ofisi ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi, kulipia gharama za huduma za umeme, mawasiliano ya simu, mitandao pamoja na kusimamia vyombo vya usafiri;

iii. Wafanyakazi nne (4) wanaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi na fani mbalimbali zikiwemo utawala wa umma, rasilimali watu, ununuzi na teknolojia ya habari na mawasiliano.

iv. Imeratibu na kusimamia utoaji wa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 49 wa Idara za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika fani na ngazi mbali mbali ndani na nje ya nchi na wafanyakazi 46 kwa mafunzo ya muda mfupi.

v. Imetayarisha na kurusha Makala maalum ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya kudumisha amani ya nchi kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 pamoja makala ya mafanikio ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa upande wa Zanzibar. Makala hayo yalirushwa kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC). Aidha, Ofisi ilitayarisha kipindi cha televisheni kilichoelezea mafanikio ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika kuadhimisha Miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Makala katika Gazeti la Zanzibar Leo. Ofisi vilevile, imeendelea kutoa taarifa za matukio mbalimbali yanayohusiana na kazi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo redio na televisheni;

vi. Imeimarisha mfumo wa ulinzi katika jengo la Ofisi Vuga kwa kukamilisha kazi ya ufungaji wa kamera za ulinzi (CCTV Camera) pamoja na kifaa cha utambuzi wa alama za vidole (Biometric Fingerprint) kwa wanaoingia katika jengo;

vii. Ofisi imeendelea kushughulikia na kufuatilia malalamiko yanayotumwa kupitia mfumo wa Sema na Rais (SNR) pamoja na kuwasiliana na wahusika wa malalamiko hayo kwa ajili ya utatuzi;

viii. Ofisi kwa kushirikiana na mamlaka ya Serikali Mtandao imeufanyia marekebisho ya mfumo wa E-office kwa Ofisi ya Uratibu na Shughuli za Serikali Dodoma sambamba na kuimarisha tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

ix. Imeendelea kutoa huduma za mikutano katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil ambapo jumla ya mikutano rasmi iliyofanyika ni 65.

**90. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii Ndogo inayotekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa Shilingi **2,641,509,000** kwa kazi za kawaida na zilizopangwa kwa kipindi cha miezi tisa ni **Shilingi 2,114,867,001.** Hadi kufikia Machi, 2026 kiasi cha fedha kilichopatikana ni **Shilingi 1,732,249,860** ambazo ni sawa na **asilimia 82** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 66** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

## Programu Ndogo – (CO10402): Mipango, Sera na Utafiti

**91. Mheshimiwa Spika;** Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na inahusika na uratibu wa masuala ya bajeti, uibuaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na masuala ya sera na tafiti zinazohusu masuala yanayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2025/2026 programu ndogo hii imetekeleza yafuatayo: -

i. Imeandaa Mpango kazi na Mpango wa Utekelezaji wa Ofisi wa mwaka 2025/2026, Taarifa ya utekelezaji wa Robo ya kwanza, Nusu Mwaka na Taarifa ya Utekelezaji ya Miezi Tisa 2025/2026 pamoja na kuandaa bajeti ya mwaka 2026/2027.

ii. Imefanya ziara 6 za ufuatiliaji wa miradi na shughuli zinazosimamiwa na Ofisi pamoja na kuandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini za mwezi na kila robo mwaka kwa mwaka 2025/2026 na kuziwasilisha Tume ya Mipango;

iii. Imeandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Ofisi kwa vipindi vya Robo mwaka 2025/2026 na taarifa nyengine za kiutendaji na kuziwasilisha katika mamlaka mbalimbali ikiwemo Tume ya Mipango na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi;

iv. Ofisi kwa kushirikiana na Idara ya Bajeti ya Wizara Fedha na Mipango imefanya mafunzo kwa Maafisa Mipango wanaohusiana na bajeti kwa ajili ya matayarisho ya Bajeti ya mwaka fedha 2026/2027;

v. Imeendelea kufuatilia uandaaji wa Sheria, Sera, Kanuni na Miongozo inayohusiana na kazi zinazosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ikiwemo Sera ya Kukabiliana na Maafa na Kanuni za Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali, Wimbo wa Taifa wa Zanzibar na Wimbo Maalum;

vi. Imeandaa na kufanya kikao cha mashirikiano baina ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) na Ofisi ya Makamu wa Rais (SJMT) ngazi ya Makatibu Wakuu pamoja na Ngazi ya Mawaziri kilichojadili masuala mbali mbali yanayohusu shughuli za Ofisi hizi;

vii. Ofisi imeandaa vikao 8 vya kutoa maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Hati mbalimbali za Mashirikiano (MoUs) baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Nchi za Nje na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa;

viii. Ofisi imeendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za Kitengo cha Uratibu na Usimamizi wa Mfuko wa Fedha wa Dunia (Zanzibar Global Funds Country Coordination Mechanism - ZGFCCM) ambacho kinaratibu na kufuatilia shughuli zote zinazofanywa na Programu za Kukabiliana na Maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria katika maeneo ya miradi kwa Unguja na Pemba;

ix. Imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais unaoendelea katika eneo la Tibirinzi Pemba.

**92. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 551,147,700** kwa kazi za kawaida na kwa miezi tisa ilipangiwa kutumia **Shilingi 400,185,900.** Hadi kufikia Machi, 2026 Idara imetumia **Shilingi 211,912,053** ambazo ni sawa na **asilimia 53** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 38** kwa fedha iliyotengwa kwa mwaka.

## Programu Ndogo – (CO10403): Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi – Pemba

**93. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba. Kwa vile shughuli zinazofanywa na Idara na Taasisi za Ofisi Unguja vilevile hutekelezwa Pemba, Programu hii inahusika zaidi na uratibu wa shughuli hizo kwa upande wa Pemba sambamba na shughuli za kiutawala za kila siku. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2025/2026. Programu ndogo hii imetekeleza yafuatayo: -

i. Imeratibu na kuhudumia ziara 14 na shughuli za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais alizozifanya kisiwani Pemba pamoja na ziara 37 za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii. Imeendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ikiwemo maslahi na stahiki za wafanyakazi 54, kulipia vifaa vya kufanyia kazi na huduma za kiuendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya Ofisi;

iii. Imeandaa Mipango ya Ofisi na bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 pamoja na kutekeleza mipango ya mwaka 2025/2026 na kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mipango hiyo ikiwemo bajeti na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa vipindi husika;

iv. Ofisi imeratibu ziara za Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Kamati ya Bajeti za Baraza la Wawakilishi zilizofanyika Pemba kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli na miradi inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba;

v. Imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Ofisi kwa upande wa Pemba ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais uliopo Tibirinzi, Chake Chake na Progamu ya TASAF;

vi. Imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo Miradi inayotekelezwa kupitia fedha za kuchochea Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo (ZCDF) na mafunzo juu ya Sheria za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo; Ukaguzi wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (CDCF) katika majimbo yote 18 ya Pemba, uzinduzi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2026 na ufanikishaji wa ratiba ya maadhimisho ya sherehe za miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwemo uwekaji wa mawe ya msingi, uzinduzi na ufunguzi wa miradi ya maendeleo;

vii. Imeratibu shughuli za kukabiliana na maafa Pemba ikiwemo kufuatilia upatikanaji wa huduma katika matukio mbali mbali ya maafa, kufanya mikutano ya wadau, kutoa elimu kwa makundi mbali mbali ya kijamii juu ya kujikinga, kujiandaa na kukabiliana na maafa, ukaguzi na ziara za ufuatiliaji katika maeneo mbali mbali, ukusanyaji wa takwimu kwa shehia zilizoathirika na maafa kuhusiana na athari za kiuchumi na fedha zinazotokana na maafa, pamoja na utoaji wa huduma, vifaa na misaada ya kibinaadamu katika maeneo yaliyopatwa na majanga;

viii. Imeratibu maandalizi ya shughuli za Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi kwa upande wa Pemba kwa kuendelea kutunza makaburi ya aliyekuwa Waziri Kiongozi Mstaafu na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Dkt. Omar Ali Juma na kaburi la aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad. Aidha, Ofisi iliratibu dua na hitma zilizofanywa kwa Viongozi wetu hao waliotangulia mbele ya haki;

**94. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi Kuu Pemba iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,184,676,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2026 imetumia **Shilingi 729,897,725** ambazo ni sawa na **asilimia 78** kwa fedha iliyotengwa kwa miezi tisa na **asilimia 62** kwa fedha zilizotengwa kwa mwaka.

Aidha, kwa upande wa makusanyo ya mapato, Programu hii ndogo ilipangiwa kukusanya **Shilingi 7,760,000** kutokana na ukodishaji wa vifaa vya sherehe na hadi Machi, 2026 ilikusanya **Shilingi 4,280,000** ikiwa ni sawa na **asilimia 55.**

## C02 – BARAZA LA WAWAKILISHI

**95. Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Baraza la Wawakilishi inatekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu mbili, ambazo ni Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali na Programu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi.

### PROGRAMU KUU - *(C0201):* KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI

**96. Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu hii ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali inahusika na uratibu wa mikutano ya Baraza la Wawakilishi ambapo lengo la Programu hii ni kuhakikisha haki na utawala wa sheria vinatekelezwa Zanzibar, ili kukuza demokrasia na uwakilishi wa wananchi. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2025/2026, Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo: -

i. Imeratibu mikutano miwili ya Baraza la Wawakilishi ambayo ni:

a. Mkutano wa Kwanza wa Baraza la 11 la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 6-10 Novemba, 2025. Mkutano huo ulikuwa maalumu kwa ajili ya uzinduzi wa Baraza jipya la 11 la Wawakilishi, ambapo shughuli kuu zilikuwa ni:

- Uchaguzi wa Mheshimiwa Spika
- Uapisho wa Wajumbe
- Uchaguzi wa Mheshimiwa Naibu Spika
- Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya uzinduzi wa Baraza jipya.

b. Mkutano wa Pili Baraza la 11 la Wawakilishi ambao ulianza tarehe 11 hadi 27 Februari, 2026. Shughuli kuu katika Mkutano huo zilikuwa ni:

- Uchaguzi wa Wenyeviti wawili wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.
- Uchaguzi wa viongozi wa Jumuiya mbali mbali za Baraza la Wawakilishi.
- Uchaguzi wa Wabunge Watano wanaoingia katika Bunge Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Baraza la Wawakilishi;
- Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora kwa mwaka wa Fedha 2023/2024.
- Taarifa ya Serikali juu ya Ripoti ya Tisa ya Utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2024/2025; na
- Taarifa ya Mwelekeo wa Mpango wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027.

ii. Imeratibu shughuli za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambapo kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025/2026 Kamati zimefanya kazi katika mizunguko miwili ya kazi za kawaida kama ifuatavyo:

a. Mzunguko wa Kwanza ulianza tarehe 13/01/2026 hadi tarehe 23/01/2026. Aidha, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo na Kamati nyengine ilifanya kazi tarehe 26/1/2026 hadi tarehe 6/01/2026;

b. Mzunguko wa Pili wa kazi za Kamati ulianza tarehe 2 hadi 20 Machi, 2026 kwa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo pamoja na Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati nyengine zilizobakia zilianza kazi kuanzia tarehe 23 Machi, 2026 hadi tarehe 10 Aprili, 2026.

**97. Mheshimiwa Spika;** Ripoti za Kamati zote za ufuatiliaji Taasisi za Serikali zitawasilishwa Baraza la Wawakilishi katika Mkutano wa mwezi wa Februari, 2027 kama Kanuni ya 124 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2024 inavyoelekeza.

## PROGRAMU KUU - (C0202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI

**98. Mheshimiwa Spika;** Programu hii ina Programu Ndogo mbili ambazo ni Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi na Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba. Lengo la Programu Kuu hii ni kuweka mazingira ya kazi yatakayowezesha Baraza la Wawakilishi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 – Machi 2026) cha mwaka wa fedha 2025/2026, Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeratibu shughuli za Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi na upatikanaji wa huduma na stahiki zote za Waheshimiwa Wajumbe na wafanyakazi wa Baraza kwa mujibu wa taratibu zilizopo;

ii. Imeendelea na maandalizi ya ujenzi wa majengo mapya ya Baraza la Wawakilishi yatakayokidhi mahitaji ya sasa na ya muda mrefu yanayotarajiwa kujengwa katika eneo la Kisakasaka Unguja;

iii. Afisi ya Baraza imeendelea na hatua za awali za kupata mfumo wa kidijitali wa kurahisisha upatikanaji wa Taarifa Rasmi za Baraza maarufu kama 'Hansard report' ambao utawezesha kubadilisha moja kwa moja mijadala ya vikao vya Baraza kutoka sauti kwenda maandishi bila ya kuchapa. Mfumo ambao utatumia akili unde (Artifitial Intelligence) unatarajiwa kurahisisha utumiaji na upatikanaji wa taarifa hizo kwa haraka kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watumiaji wengine;

iv. Afisi pia, imeanza hatua ya awali ya kufanya mawasiliano na Taasisi za Kitaalamu kuhusu uandaaji wa Mfumo wa Kiteknolojia wa kusimamia na Kutathmini Miswada ya Sheria inayowasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa kupitishwa;

v. Afisi ya Baraza imetoa vipindi **11** vya elimu kwa umma kuhusu shughuli za Baraza la Wawakilishi kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC);

vi. Katika kutangaza historia na shughuli za Baraza, Afisi ya Baraza la Wawakilishi ilishiriki maonyesho ya **12** ya Biashara yaliyofanyika katika Viwanja vya Maonyesho ya Biashara Dimani-Unguja kuanzia tarehe 29 Disemba, 2025 hadi tarehe 16 Januari, 2026 ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 62 ya Mapinduzi Zanzibar ya mwaka 1964. Aidha, Afisi ya Baraza ilishiriki maonyesho ya siku ya Sheria yaliyofanyika katika Uwanja wa Gombani ya Kale - Pemba, tarehe 5 hadi 8 Februari, 2026;

vii. Afisi ilitoa mafunzo kwa Waandishi wa Habari wanaoripoti shughuli za Baraza kuhusu taratibu za msingi za Shughuli za Baraza;

viii. Afisi imeendelea kuwajengea uwezo watendaji wake ambapo jumla ya watendaji **17** wameendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali. Vilevile, watendaji 90 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi.

ix. Afisi pia, imewapatia mafunzo mbali mbali ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

**99. Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Programu zake Kuu mbili kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 34,770,000,000** kwa matumizi ya kawaida na hadi kufikia Machi 2026, Afisi imetumia **Shilingi 20,460,908,871** sawa na **asilimia 91.6** kwa fedha iliyopangwa miezi tisa na **asilimia 58.9** kwa mwaka.

**C03 – TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR**

**100. Mheshimiwa Spika;** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kuendesha mwenendo mzima wa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar ikihusisha kusimamia, kukuza na kuratibu elimu ya wapiga kura, kuandaa, kuhifadhi na kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga kura, kufanya mapitio ya mipaka, idadi na majina ya Majimbo ya Uchaguzi na kuendesha Kura ya Maoni Zanzibar. Jukumu hili linatekelezwa kupitia Programu Kuu mbili ambazo ni Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

## PROGRAMU KUU - (C0301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI

**101. Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu hii inatekeleza jukumu la msingi la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo ni kuratibu na kusimamia chaguzi mbalimbali za nchi. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 – Machi 2026) cha mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Uchaguzi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo: -

i. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliendesha zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya wapiga kura wapya walioandikishwa katika uandikishaji wa awamu ya kwanza na ya pili zilizofanyika Disemba 2024 na Februari 2025. Zoezi hilo lilifanyika katika vituo vya uandikishaji vya Unguja na Pemba kwa muda wa siku mbili kuanzia tarehe 30 hadi 31 Agosti 2025. Aidha, Afisi ya Tume iliendeleza shughuli za uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kupokea na kuweka wazi maombi ya wapiga kura wanaohamisha taarifa zao kutoka eneo moja kwenda jengine pamoja na kuwafuta wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo katika Daftari la Kudumu la Wapiga kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar;

ii. Tume iliendelea kutoa elimu ya wapiga kura kwa makundi mbalimbali ya kijamii ili kuwawezesha kufahamu haki yao ya kupiga kura na kujua mchakato mzima wa uchaguzi. Jumla ya wananchi 1,904, wanawake wakiwa 1,006 na wanaume 898 walipatiwa elimu kupitia makundi mbali mbali katika shehia zote za Unguja na Pemba. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ilitumia vyombo vya habari mbalimbali kutoa elimu hiyo vikiwemo ZEC Online TV, ZBC, Asam Online TV, Katiba Online TV na Azam TV. Vilevile, Tume ilitoa machapisho mbali mbali ya shughuli za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 yakiwemo maandishi ya nukta nundu kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu wa uoni ili kuwawezesha kupata fursa ya kupiga kura bila ya kutegemea msaada wa mtu mwengine.

   Elimu hii pia ilitolewa kwa njia ya matangazo kupitia mitandao ya kijamii, gari la matangazo ya barabarani ambalo lilipita mijini na vijiji vyote vya Unguja na Pemba, matamasha ya kimichezo, kugawa vipeperushi na kujibu masuala ya wananchi kuhusiana na uchaguzi na kupitia taasisi mbalimbali za elimu na skuli za sekondari ili kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mchakato wa uchaguzi na kutekeleza haki ya kupiga kura.

iii. Tume iliendesha mafunzo ya wadau na watendaji wa uchaguzi juu ya uendeshaji wa uchaguzi wakiwemo Wasimamizi wasaidizi 100 wa majimbo, Watendaji wa Vyombo vya Habari vya Umma na Binafsi na Wagombea wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi wa majimbo na viti maalumu kwa Unguja na Pemba. Tume ya Uchaguzi ilitoa mafunzo maalum kwa watu wasioona juu ya matumizi ya "Tactile ballot" ili kuliwezesha kundi hili kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kupiga kura kwa uhuru, usiri na usahihi.

Vilevile, Tume iliandaa na kutoa mafunzo kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama juu ya jukumu lao la kuhakikisha kuwa uchaguzi unafanyika kwa njia ya amani na utulivu. Pia ilindesha mafunzo kwa watendaji wa vituo 1,752 vya upigaji kura vya Unguja na Pemba wakiwemo Wakuu wa Vituo vya Kupigia Kura (POs), Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo Nam. 1 na 2 (PAs), Waratibu wa Maeneo ya Kupigia Kura (OPO) na makarani wanaoongoza Mistari (DC);

iv. Afisi ya Tume ya Uchaguzi iliendesha mikutano ya wadau mbalimbali wa uchaguzi ikiwa ni maandalizi ya ushiriki wao katika Uchaguzi Mkuu wa 2025. Miongoni mwa mikutano hiyo ni Mikutano ya Kamati za Ushauri za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Mikutano ya Wadau ngazi za Wilaya ambayo iliendeshwa na Afisi za Uchaguzi za Wilaya zote za Zanzibar, Mikutano ya kutathmini Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 iliyohusisha Tume na Wafanyakazi wa Tume ya Uchaguzi, Tume na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo kwa majimbo yote 50 ya Uchaguzi na Mkutano wa Tume na Wadau wa Uchaguzi;

v. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilitoa Vibali vya Uangalizi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ambapo jumla ya asasi za kiraia 56 zenye jumla ya waangalizi 1,123 kwa waangalizi wa ndani na Taasisi za nje 14 zikiwa na jumla ya waangalizi 28 zilipatiwa vibali hivyo. Hatua hii ni sehemu ya jitihada za Tume kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na imani na Tume kwa kuelewa kuwa Tume inafanya kazi kwa uwazi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria;

vi. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliendesha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 tarehe 29 Oktoba 2025, kwa salama na amani. Uchaguzi huu ulihusisha uchaguzi wa Kiti cha Urais ambapo jumla ya wagombea 11 waligombea, uchaguzi wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi wagombea 484 na Udiwani

wagombea 341. Idadi ya Wapiga kura waliojitokeza kupiga kura ni 609,096 ambayo ni sawa na asilimia 84.88 ya waliojiandikisha.

vii. Tume ya Uchaguzi baada ya kukamilika kwa utoaji wa matokeo ya Uchaguzi iliwateua wajumbe 20 wa viti maalum kwa wanawake katika Baraza la Wawakilishi kutoka katika vyama viwili vilivyopata viti katika Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa mwaka 2025. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 67 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kifungu cha 53(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2018. Chama cha Mapinduzi kilipata jumla ya viti 16 na Chama cha ACT Wazalendo kilipata viti vinne (4). Vile vile, Tume iliteua Madiwani wa viti maalum wanawake 43 katika Mamlaka zote 11 za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa idadi ya viti vilivyopata vyama vyao katika Uchaguzi;

viii. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilianza kusimamia mashauri mbali mbali yaliyofunguliwa ya kupinga matokeo ya Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani katika Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa mwaka 2025 ambapo jumla ya mashauri 26 yaliwasilishwa katika Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa matokeo ya kiti cha Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na ombi moja la kiti cha Udiwani. Katika mashauri hayo, tisa (9) yamefunguliwa katika Masjala ya Mahakama Kuu ya Chakechake Pemba na mashauri 17 yamefunguliwa katika Masjala ya Mahakama Kuu ya Tunguu. Hadi kumalizika kwa mwezi wa Machi 2026, mashauri tisa (9) ya Pemba na nane (8) ya Unguja yaliondolewa kwa hatua ya mwanzo baada ya kusikilizwa na kutupiliwa mbali na Mahakama Kuu. Hata hivyo, mashauri hayo kwa sasa yanaendelea katika hatua za Rufaa na mengine tisa (9) yapo katika hatua ya kusikilizwa;

ix. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliteketeza nyaraka za Uchaguzi wa Oktoba 29, 2025 ikiwa ni utekelezaji wa kifungu 98(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2018. Zoezi hilo ambalo lilifanyika tarehe 8 Febuari, 2026 kwa upande wa Pemba na tarehe 28 Febuari, 2026 kwa upande Unguja lilihusisha Mamlaka mbalimbali zikiwemo Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Idara ya Mazingira, Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu pamoja na wadau wengine wa Uchaguzi.

## PROGRAMU KUU - (CO302): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

**102. Mheshimiwa Spika;** Programu hii Kuu inahusika na uwekaji wa mazingira mazuri kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kutekeleza majukumu yake. Katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 – Machi 2026) cha mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Uchaguzi kupitia Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeshiriki katika Mkutano uliohusisha nchi zilizoendesha Uchaguzi Mkuu kwa mwaka 2025 ili kutoa taarifa kuhusu namna chaguzi zao zilivyokuwa. Jukwaa hili ni sehemu ya kuimarisha mahusiano mazuri na Taasisi nyengine za ndani na nje ya Nchi;

ii. Afisi ya Tume imeendelea kuimarisha upatikanaji huduma zinazotolewa kwa kununua vifaa vya ofisi na kulipia huduma mbalimbali ikiwemo, umeme na intaneti;

iii. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Afisi za Uchaguzi za Wilaya za Kaskazini "A", Kaskazini "B" na Kati kwa Unguja na Wilaya za Micheweni na Mkoani kwa upande wa Pemba. Mradi huu umelenga kuziwezesha Afisi za Wilaya za Uchaguzi kuweza kutoa huduma kwa wadau wake kwa ukaribu na katika mazingira yaliyo bora. Ujenzi wa Afisi hizo unaendelea katika hatua tofauti na unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi sita kwa kila Wilaya;

iv. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeendelea kuwaendeleza kimasomo wafanyakazi wake katika kada na fani mbali mbali ili kuwaongezea ujuzi na uweledi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Jumla ya wafanyakazi sita (06) wanaendelea na masomo ya muda mrefu wakiwemo wanawake watano, watatu Shahada ya Kwanza na wawili Shahada ya Pili na mwanaume mmoja ambae anaendelea na Shahada ya Pili.

**103. Mheshimiwa Spika;** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kupitia Programu zake Kuu mbili kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iliidhinishiwa kutumia jumla ya S**hilingi 6,016,500,000** kwa matumizi ya kawaida na kwa robo tatu ya mwaka ilipanga kutumia **Shilingi 4,495,806,627.97**. Hadi kufikia Machi 2026, Afisi imetumia jumla ya

**Shilingi 3,587,737,082.05** sawa na **asilimia 79.80** kwa fedha iliyopangwa miezi tisa na **asilimia 59.63** kwa fedha iliyopangwa kwa mwaka.

**104. Mheshimiwa Spika;** Vilevile, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilipangiwa kukusanya **Shilingi 60,105,467** na hadi kufika Machi 2026, fedha zilizokusanywa ni **Shilingi 156,100,000** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 159.7** ya fedha zilizotengwa kukusanywa kwa mwaka. Fedha hizo zimeingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

## UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI 2025/2026)

**105. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeendelea kutekeleza miradi minne ya maendeleo. Utekelezaji wa kazi za Miradi hiyo katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 – Machi 2026) ni kama ifuatavyo:-

### 1. Mradi wa Kujenga Uhimili wa Kukabiliana na Maafa

**106. Mheshimiwa Spika;** Mradi huu unatekelezwa na Kamisheni ya Kukabiliana Maafa na fedha zake zinatoka kwa Wahisani hasa mashirika ya Umoja wa Mataifa UNICEF na WFP kwa madhumuni ya kujenga uwezo wa taasisi kutekeleza majukumu yake. Mradi huu katika kipindi hiki umetekeleza kazi zifuatazo:

i. Imeratibu na kuandaa vikao vinne (4) vilivyowahusisha wadau wa kukabiliana na maafa Unguja na Pemba kujadili mafanikio na changamoto pamoja na kuweka mikakati ya kutatua changamoto hizo katika kukabiliana na maafa katika maeneo yao;

ii. Imekamilisha hatua za awali za kuandaa Mfumo wa Pamoja wa Taarifa za Maafa (ZDMIS) utakaorahisisha shughuli mbali mbali za kukabiliana na maafa ikiwemo utoaji wa elimu na tahadhari za mapema, kutuma na kupokea taarifa za Maafa na kuwawezesha wadau kukabiliana na maafa kwa ufanisi mkubwa zaidi pamoja na kununua baadhi ya vifaa vya mfumo huo;

iii. Imewajengea uwezo Makatibu Wakuu wa Wizara zote za SMZ ambao ni wajumbe wa Kamati ya Kitaalam ya Kukabiliana na Maafa kwa kuwapatia mafunzo ya masuala ya kukabiliana na maafa kwa lengo la kuelewa dhana nzima ya maafa na majukumu yao wakiwa ni wadau muhimu katika masuala ya kukabiliana na maafa nchini;

iv. Imetoa mafunzo ya tahadhari za mapema kwa makundi saba (7) yaliyo katika mazingira hatarishi ya kuathiriwa na Maafa kwa Unguja na Pemba, wakiwemo watu wenye mahitaji maalumu, wavuvi, wanawake na vijana, wazee, wafugaji na wakulima, waendesha bodaboda na bajaji na watu wanaoishi maeneo hatarishi;

v. Ofisi imekamilisha hatua za awali za kuandaa Mfumo wa Pamoja wa Taarifa za Maafa (ZDMIS) utakaorahisisha shughuli za kukabiliana na maafa ikiwemo utoaji wa elimu na tahadhari za mapema, kutuma na kupokea taarifa za maafa na kuwawezesha wadau kutekeleza majukumu yao kwa wakati na ufanisi zaidi;

vi. Ofisi imeendelea kuimarisha Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura kwa kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kituo vikiwemo "drone" moja, "multi-media projector", "Laptop" tatu (3) "leser printer" moja (1) na "desktop computer" mbili (2) vyenye gharama ya Shilingi Milioni 100. Vifaa hivyo vinatarajiwa kuwasili Zanzibar baina ya mwezi Mei na Juni mwaka huu na vimegharamiwa na Shirika la Chakula Duniani (WFP).

**2. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III)**

**107. Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao kwa awamu ya tatu ulikamilika mwezi Septemba 2025. Kabla ya kukamilika kwake kwa awamu hii shughuli zifuatazo zimetekelezwa:

i. Imeratibu na kusimamia zoezi la majaribio la Uibuaji wa Walengwa wa kaya Masikini, ambalo lilifanyika kwa Shehia **75** kwa Unguja na Pemba zenye idadi ya Kaya **13,919** (Unguja **899** na Pemba **13,020**). Madhumuni ni kupata taarifa za Shehia zilizokuwa na viashiria vya umasikini kutokana na mabadiliko ya tabianchi;

ii. Imetoa Ruzuku ya Uzalishaji ya **Shilingi 41,994,281** kwa Kaya za Walengwa **135** wa Unguja;

iii. Imeratibu na kusimamia malipo ya Kaya Masikini, ambapo jumla ya **Shilingi 1,750,993,473** zimelipwa kwa Kaya **27,886** za Unguja na Pemba;

iv. Ofisi imekamilisha ujenzi wa madarasa **19** ya Skuli tatu ambazo ni Skuli ya Kendwa (madarasa **7**), Skuli ya Mtangani (madarasa **5**) na Skuli ya Dodo (madarasa **7**). Ujenzi huo umegahrimu **Shilingi 347,526,500.**

**3. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya makaazi ya Makamu wa Pili wa Rais, Tibirinzi Pemba**

**108. Mheshimiwa Spika;** Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Makaazi ya Makamu wa Pili wa Rais, Tibirinzi Pemba umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha na kuweka mazingira mazuri ya makaazi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kuwa na makaazi yanayoendana na hadhi yake. Mradi huu ulianza rasmi mwezi Mei 2025 na umepangwa kukamilika mwezi Novemba, 2026 ikiwa ni kipindi cha miezi 18. Ujenzi huu unahusisha jengo kuu la makaazi lenye ghorofa mbili (G+2+R) pamoja na majengo saidizi ikiwemo ukuta (fence), nyumba za ulinzi (guard house) na uwekaji sawa ardhi (landscaping). Hatua ya ujenzi iliyofikiwa hadi mwezi Machi, 2026 ni **asilimia 58** ya utekelezaji halisi wa kazi.

**109. Mheshimiwa Spika;** Mradi huu umekisiwa kutumia **Shilingi 5,397,223,989** (pamoja na VAT) na kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mradi uliidhinishiwa kutumia **Shilingi 2,000,000,000** ambapo hadi Mwezi Machi 2026 fedha iliyotumika ni **Shilingi 1,853,259,673** sawa na **asilimia 93** ya fedha iliyotengwa.

**4. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Ghala la Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, Kisakasaka**

**110. Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais vilevile, inaratibu ujenzi wa Ofisi na Ghala la Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa unaoendelea katika eneo la Kisakasaka, Wilaya ya Magharibi B. Ujenzi huu unahusisha jengo la Ofisi na ghala la kisasa la kuhifadhia vifaa vya operesheni na huduma za kibinadamu, kituo cha operesheni na mawasiliano ya dharura (Emergency Operation Centre), kituo cha kufuatilia majanga (Situation room), kituo cha mawasiliano ya dharura (National Calling Centre) na kituo cha mafunzo ya masuala ya maafa (training centre). Ujenzi hivi sasa upo katika hatua za msingi (base) na gharama za ujenzi zinasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

**5. Mradi wa Ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dodoma lililopo Dar es Salaam**

**111. Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika mwaka wa fedha, 2025/2026 ilipanga kutekeleza Mradi wa Ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Uratibu wa

Shughuli za SMZ lililopo Dar es Salaam kwa lengo la kulifanyia matengenezo makubwa jengo hilo ili liendane na mazingira ya eneo lililopo na hadhi yake. Ofisi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 550,000,000** kwa Mradi huo ambao hatua ya utekelezaji wake hivi sasa ni kufanya majadiliano (negotiation) na Mkandarasi aliyeshinda zabuni. Ofisi imepanga kuingia mkataba na Mkandarasi huyo ndani ya mwezi Aprili, 2026.

## UTEKELEZAJI KIFEDHA

**112. Mheshimiwa Spika;** kwa ujumla Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 120,896,500,000** ambapo **Shilingi 82,912,500,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 37,984,000,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Ofisi imetumia **Shilingi 56,727,353,334** kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na **asilimia 94** kwa fedha zilizopangwa kutumika kwa miezi tisa na **asilimia 68** fedha zilizopangwa kutumika kwa mwaka. Kadhalika, kwa upande wa kazi za maendeleo, Ofisi imepata S**hilingi 4,383,773,929** ikiwa ni **asilimia 15** ya kiasi kilichopangwa kwa miezi tisa na **asilimia 12** kwa fedha zilizopangwa kwa mwaka. Kati ya fedha zilizopatikana **Shilingi 2,455,514,256** ni mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **Shilingi 75,000,000** ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar **(Kiambatisho Nam. 3 na Nam. 4).**

**113. Mheshimiwa Spika;** vilevile, Ofisi ilipangiwa kukusanya **Shilingi 95,105,647** na hadi kufikia Machi 2026, fedha zilizokusanywa ni **Shilingi 180,355,000** sawa na **asilimia 202** ya fedha zilizotengwa kukusanya kwa miezi tisa na asilimia 190 ya fedha zilizotengwa kukusanya kwa mwaka **(Kiambatisho Namba 5)**.

## MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**114. Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na taasisi zake kwa mwaka 2026/2027 itaendelea kutekeleza na kusimamia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo **14** katika mafungu matatu ya kibajeti. Mafungu hayo kuanzia mwaka wa fedha 2026/2027 yatakuwa yanajulikana kama ifuatavyo:

i. 003 – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (zamani C01)

ii. 020 – Baraza la Wawakilishi (zamani C02)

iii. 031 – Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (zamani C03)

**115. Mheshimiwa Spika;** kupitia Programu na Mafungu hayo ya kibajeti, Ofisi imepanga kutekeleza yafuatayo: -

**Fungu 003 – OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

## PROGRAMU KUU - (P03): URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS

### Programu Ndogo (S0301): Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais

**116. Mheshimiwa Spika;** Program hii ina Programu Ndogo moja ya Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais ina lengo la kuimarisha utendaji wa kazi kwa Ofisi ya Faragha na kutoa huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi kupitia Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais imepanga kufanya yafuatayo: -

i. Kuratibu ziara 60 za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais za ndani ya nchi na ziara 2 za nje ya nchi;

ii. Kuimarisha mashirikiano na mahusiano mema ya kitaifa na kimataifa kwa kuandaa vikao baina ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na Mabalozi pamoja na Wageni Mashuhuri kutoka nchi za nje na mashirika na jumuiya za kikanda na kimataifa;

iii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais zinazolenga kuleta maendeleo katika jamii;

iv. Kuyafanyia kazi malalamiko, migogoro na kero za wananchi kwa kushirikiana na taasisi husika;

v. Kufanya matengenezo ya kawaida katika makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais yalioko Dodoma, Unguja na Pemba;

vi. Kuratibu vikao vya uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Wizara zote za SMZ ambavyo vitafanyika kila baada ya miezi mitatu.

vii. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi saba (7) wa Ofisi ya Faragha kwa kiwango cha Stashahada, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Pili pamoja na kuwapatia stahiki nyengine wafanyakazi wa Afisi ya Faragha.

**117. Mheshimiwa Spika;** ili Programu hii ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais itekeleze kazi zake kwa mwaka 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 2,265,376,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,639,384,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na michango inayoambatana nayo na **Shilingi 625,992,000** ni kwa matumizi mengineyo.

## PROGRAMU KUU - (P02): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

**118. Mheshimiwa Spika;** lengo la Programu hii ni kuweka mfumo imara na endelevu wa uratibu wa shughuli za Serikali, ambapo matarajio ya muda mrefu ni kupatikana kwa huduma bora za Serikali kwa jamii. Programu hii ina Programu Ndogo nne (4) ambazo ni Kukabiliana na Maafa, Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Uratibu wa Shughuli za SMZ Dodoma.

### Programu Ndogo – S0201: Kukabiliana na Maafa

**119. Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina lengo la kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa kabla, wakati na baada ya kutokea. Kazi za Programu ndogo hii zinatekelezwa na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar.

Katika mwaka wa fedha 2026/2027, kupitia fedha za kawaida kutoka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kamisheni imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuratibu utoaji wa huduma na misaada ya kibinaadamu katika matukio 300 ya majanga/ maafa yanayoweza kutokea Unguja na Pemba;

ii. Kuimarisha mfumo wa mawasiliano ya dharura, mfumo wa taarifa za usimamizi wa maafa (ZDMIS) pamoja na kutoa tahadhari za mapema kwa wadau na jamii kwa ujumla;

iii. Kufanya kaguzi 66 Unguja 36 na Pemba 30 za uwepo wa utendaji kazi wa mipango na taratibu za kukabiliana na maafa katika taasisi na maeneo mbali mbali kwa mujibu wa muongozo wa ukaguzi unavyoelekeza;

iv. Kufanya vikao viwili (2) vya tathmini na ufuatiliaji wa ripoti ya kutuama kwa maji ya mvua na utiririshaji wa maji machafu ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

v. Kuandaa mikutano na wahusika wa Kukabiliana na Maafa kwa mujibu wa Sheria na Miongozo inavyoelekeza;

vi. Kuandaa na kuchapisha miongozo mbalimbali ya kukabiliana na maafa;

vii. Kufanya ufuatiliaji na tathimini kwa shughuli za kukabiliana na Maafa zinazotekelezwa na Kamisheni;

viii. Kuwajengea uwezo wadau wa masuala ya maafa katika ukusanyaji takwimu za majanga na maafa pamoja na kukusanya na kufanya uchambuzi wa takwimu mbali mbali za matukio ya majanga na maafa yanayoweza kutokea;

ix. Kufanya zoezi la kupima utayari (simulation exercise) kwa wadau wa maafa

x. Kutoa elimu ya kujikinga na kukabiliana na maafa kwa jamii na wadau mbalimbali zikiwemo taasisi za Serikali na binafsi;

xi. Kufanya vikao viwili (2) vya Kamisheni na vikao viwili (2) vya Kamati ya Kitaalam ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa

xii. Kufanya Kongamano la masuala ya maafa pamoja na kuadhimisha siku ya Kimataifa ya Kukabiliana na Maafa kwa 2027 pamoja na kushiriki katika maadhimisho mengine ya kitaifa

xiii. Kufanya tathmini ya athari za majanga na maafa kwa upande wa kiuchumi na kifedha

xiv. Kufanya vikao vinne (4) vya uratibu wa Mpango wa Taifa wa Afya Moja katika kukabiliana na majanga yanayojitokeza pamoja na kufanya ziara kwa taasisi zinazotekeleza masuala ya afya moja

xv. Kuchambua na kuandaa ramani za maeneo hatarishi kwa Wilaya ya Kusini Unguja

xvi. Kuwapatia wafanyakazi mishahara na stahiki zao;

xvii. Kuratibu shughuli za uendeshaji na utawala wa Kamisheni; na

xviii. Kuwajengea uwezo watendaji wa Kamisheni kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

**120. Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa kazi za kawaida kupitia fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo; Ofisi kupitia Programu Ndogo hii ya Kukabiliana na Maafa imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupunguza Athari za Maafa Duniani kwa mwaka 2026;

ii. Kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Kukabiliana na Maafa (ZDMIS);

iii. Kuimarisha kazi za kukabiliana na maafa kwa kila robo mwaka;

iv. Kutoa taarifa za tahadhari za mapema kwa makundi ya jamii yanayoweza kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

**121. Mheshimiwa Spika;** ili Programu ndogo ya Kukabiliana na Maafa itekeleze kazi zake kwa mwaka 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 3,083,058,000** ikiwa ni ruzuku kwa matumizi ya kazi za kawaida kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,040,610,000** ni ruzuku kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 1,742,020,000** ni ruzuku kwa matumizi mengineyo. Aidha, naliomba Baraza liidhinishe **Shilingi 300,428,000** kwa matumizi mengineyo kupitia fedha za washirika wa maendeleo.

## Programu Ndogo – S0202: Kusimamia Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa

**122. Mheshimiwa Spika;** Programu hii Ndogo ina jukumu la kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Kazi za Programu hii zinatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi kupitia Programu ndogo hii imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuratibu Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 63 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964;

ii. Kuratibu ushiriki wa wananchi na Viongozi katika Maadhimisho ya Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara pamoja na Siku ya Mashujaa;

iii. Kuratibu Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi na Siku ya Kumbukumbu ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume;

iv. Kuratibu na kuandaa banda la kumbukumbu ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume katika maonesho ya Kumbukizi ya Baba wa Taifa na Wiki ya Vijana wakati wa kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa;

v. Kununua vifaa vya sherehe ikiwemo, mashamiana, viti, meza na bendera kwa ajili ya Sherehe za Kitaifa;

vi. Kuendelea kukusanya mapato yasiyo ya kodi kwa kukodisha maduka na vifaa vya sherehe;

vii. Kuwapa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi wa Idara ya Sherehe na Maadhimisho Kitaifa;

viii. Kuimarisha utendaji wa Ofisi kwa kununua vifaa mbali mbali vya kufanyia kazi vikiwemo karatasi, mafuta na vifaa vya kuandikia.

**123. Mheshimiwa Spika;** ili Programu ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa itekeleze kazi zake kwa mwaka 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 2,225,694,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi 402,530,000** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 1,823,164,000** kwa matumizi mengineyo.

## Programu Ndogo – S0203: Kusimamia Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

**124. Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo hii ina jukumu la kuratibu shughuli za SMZ, mambo ya muungano, utafiti kitaifa pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) hapa Zanzibar. Programu hii ndogo inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, katika mwaka wa fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za SMZ ikijumuisha mipango ya kisekta mtambuka, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2025 na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

ii. Kuratibu na kusimamia Masuala ya Muungano kupitia vikao vya Kisekta vya masuala ya Muungano na utatuzi wa Hoja za Muungano; ushirikiano baina ya Wizara na Taasisi za SMZ na SJMT; Shughuli za Taasisi na Miradi ya Muungano Zanzibar; Miradi ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo; na Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Masuala ya Muungano.

iii. Kuratibu Masuala ya Sera na Siasa kwa kuratibu shughuli za Kisiasa; Utekelezaji wa Sera za Kisekta; Uandaaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Amani kwa Vijana na Maendeleo Endelevu; na Kuratibu Shughuli za Baraza la Wawakilishi.

**125. Mheshimiwa Spika;** Ofisi vilevile, itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini TASAF; na utekelezaji wa Shughuli za Idara ya Uhamiaji Zanzibar kwa kuimarisha utoaji wa huduma kwa raia na wageni pamoja na kukamilisha miradi ya maendeleo.

**126. Mheshimiwa Spika;** ili Programu Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itekeleze kazi zake kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 77,299,903,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 821,374,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara, S**hilingi 3,690,929,000** kwa matumizi mengineyo ya Idara, **Shilingi 32,687,600,000** kwa ajili ya ruzuku ya matumizi mengineyo ya Idara ya Uhamiaji, **Shilingi 100,000,000** ni mchango wa SMZ katika shughuli za TASAF na **Shilingi 40,000,000,000** ni fedha za maendeleo ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo kwa Programu ya TASAF.

**Programu Ndogo – S0204: Kusimamia Shughuli za SMZ Dodoma**

**127. Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo ya Shughuli za SMZ Dodoma ina lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali/Taasisi za SMZ na SJMT, Washirika wa Maendeleo, Afisi za Kibalozi na asasi nyengine za kimataifa. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Programu hii Ndogo imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuratibu upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanapokuwa Tanzania Bara ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na ufanisi ikiwemo usafiri na upatikanaji wa VISA;

ii. Kutoa elimu juu ya uwepo wa Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma kwa kufanya warsha 1 kwa wadau, kufanya kongamano la Maadhimisho ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964, kuhudhuria katika Tamasha la Kimataifa la Biashara wakati wa Maadhimisho ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tamasha la Biashara la Saba Saba, Tamasha la Kilimo Nane Nane na kufanya vipindi viwili (2) vya Televisheni ya ZBC;

iii. Kufanya utafiti wa kutathmini utaoji wa huduma za Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma;

iv. Kuratibu na kushiriki vikao 80 vya Ofisi na Wizara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi nane (8) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi;

vi. Kuwapatia wafanyakazi stahiki zao zikiwemo likizo, malipo ya baada ya saa za kazi na malipo ya mazishi.

**128. Mheshimiwa Spika;** ili Programu Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Dodoma itekeleze kazi zake kwa mwaka 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 2,465,208,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 820,627,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 1,644,581,000** kwa matumizi mengineyo.

## PROGRAMU KUU - (P01): UTAWALA NA UENDESHAJI WA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

**129. Mheshimiwa Spika;** lengo la Programu hii ni kuimarisha mazingira bora ya wafanyakazi, usimamizi wa mipango na shughuli za Ofisi ili kutoa huduma bora kwa jamii. Programu hii kuu ina Programu Ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi, Pemba.

### Programu Ndogo – S0101: Utawala na Uendeshaji

**130. Mheshimiwa Spika;** Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kusimamia na kuweka mazingira bora ya kazi na kutoa huduma bora za uendeshaji za kila siku pamoja na kusimamia rasilimali za Ofisi na maslahi ya wafanyakazi. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Programu hii Ndogo pamoja na mambo mengine, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuendelea kusimamia maslahi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao zikiwemo za mshahara, likizo na stahiki nyengine kwa mujibu wa miongozo ya kiutumishi;

ii. Kuimarisha shughuli za uendeshaji wa ofisi zikiwemo za usafiri, mawasiliano, gharama za umeme, maji na vitendea kazi;

iii. Kuratibu na kusimamia vikao vya kiutendaji vya Ofisi vikiwemo vikao vya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi;

iv. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi 10;

v. Kuratibu zoezi la upimaji afya kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

vi. Kufanya upanuzi, ukarabati na uwekaji wa vitendea kazi vya kisasa katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil;

vii. Kuimarisha kituo cha uwekaji kumbukumbu za Ofisi pamoja na kuanzisha maktaba.

**131. Mheshimiwa Spika;** ili Programu ndogo ya Uongozi na Utawala itekeleze kazi zake kwa mwaka 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 2,810,764,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,277,480,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara, na **Shilingi 1,533,284,000** kwa matumizi mengineyo.

## Programu Ndogo – S0102: Mipango, Sera na Utafiti

**132. Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti inahusika na kuandaa na kusimamia mipango na bajeti na pamoja na kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu Ndogo hii imepanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti, mipango pamoja na miradi ya maendeleo ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na 2027/2028;

ii. Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Programu/miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Idara/Taasisi zilizozo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na kazi za kawaida za Ofisi;

iii. Kuratibu uandaaji na mapitio ya Sera, Sheria na Miongozo inayohusu shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

iv. Kuratibu na kuandaa Vikao vya Mashirikiano baina ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

v. Kujenga uwezo kwa Maafisa Ufuatiliaji na Tathmini na Maafisa Mipango wa Idara/Taasisi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais juu ya kazi wanazozisimamia na kuzitekeleza;

vi. Kuratibu na kusimamia na kufanya tafiti zinazohusiana na sekta zilizomo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

vii. Kufanya mapitio ya nyenzo za kukusanyia taarifa za takwimu za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

viii. Kuratibu na kuandaa nyaraka za Ofisi kwa ajili ya matumizi mbalimbali;

ix. Kusimamia shughuli za Kitengo cha Uratibu na Usimamizi wa Kitaifa wa Mfuko wa Fedha wa Dunia (ZGFCCM).

**133. Mheshimiwa Spika;** ili Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti itekeleze kazi zake kwa mwaka 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 912,847,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 335,227,000** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 577,620,000** kwa matumizi mengineyo. Aidha, **Shilingi 204,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya shughuli za Uratibu na Usimamizi wa Kitaifa wa Mfuko wa Fedha wa Dunia (ZGFCCM) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

## Programu Ndogo – S0103: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi – Pemba

**134. Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba inahusika na kuratibu shughuli za Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba na kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi kwa jumla. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Programu hii Ndogo imepanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba;

ii. Kuratibu ziara na shughuli za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Pemba;

iii. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi kumi na moja (11) wa Ofisi;

iv. Kuandaa mipango ya Ofisi na kusimamia utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

v. Kuimarisha kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Program na Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba;

vi. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali Pemba;

vii. Kuratibu shughuli za kukabiliana na maafa na kutoa elimu kwa jamii juu ya kujikinga, kujiandaa na kukabiliana na maafa Pemba;

viii. Kuratibu shughuli za sherehe na maadhimisho ya kitaifa na shughuli za kuwaenzi viongozi wakuu wa kitaifa Pemba;

**135. Mheshimiwa Spika;** ili Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba itekeleze kazi zake kwa mwaka 2026/2027, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 1,252,878,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi 819,588,000** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 433,290,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

## FUNGU 020 – BARAZA LA WAWAKILISHI

**PROGRAMU KUU - (PO1): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI NA PROGRAMU KUU - (PO2): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**136. Mheshimiwa Spika;** Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali ina jukumu la kuhakikisha haki na utawala wa sheria unatelekelezwa Zanzibar. Matarajio yake ya muda mrefu ni kukua kwa demokrasia na uwakilishi wa wananchi katika kusimamia na kufuatilia shughuli za Serikali. Huduma zinazotolewa na Programu hii ni kujadili, kurekebisha na kupitisha miswada ya Sheria, kusimamia utendaji wa taasisi za Serikali na kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali.

**137. Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi inahusika na kuweka mazingira mazuri ya kazi, kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza ili kuongezeka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Baraza na Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa jumla.

**138. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027, Programu hizi Kuu ambazo shughuli zake zinatekelezwa na Afisi ya Baraza la Wawakilishi zimepanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kuratibu Mikutano minne (4) ya kila mwaka ya Baraza la Wawakilishi;

ii. Kuratibu shughuli za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi;

iii. Kuendelea kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza ili kukuza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao;

iv. Kutoa taaluma kwa umma kuhusu shughuli za Baraza kupitia vipindi vya Redio na Televisheni;

v. Kuratibu shughuli za Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi ili iweze kusimamia majukumu yake yanayohusu Utumishi wa Baraza;

vi. Kuendelea kuimarisha mazingira ya Baraza kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya majengo ya Afisi ya Baraza na nyumba za makaazi ya Mheshimiwa Spika;

vii. Kuanza utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Majengo mapya ya Baraza la Wawakilishi katika eneo la Kisakaska - Unguja;

viii. Kuendeleza mifumo ya kidijitali ili kuongeza ufanisi wa kazi.

**139. Mheshimiwa Spika;** ili Afisi ya Baraza la Wawakilishi iweze kutekeleza malengo yake hayo kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 kwa ufanisi zaidi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe **Shilingi 36,849,650,000** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 12,672,758,608** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 24,176,891,392** ni kwa matumizi mengineyo.

## FUNGU 031 – TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

**140. Mheshimiwa Spika;** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2026/2027 itaendelea kutekeleza Programu zake Kuu mbili ambazo ni Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Programu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala za Uendeshaji wa shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

### PROGRAMU KUU - (P03101): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI

**141. Mheshimiwa Spika;** Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi inahusika na kupanga na kutekeleza jukumu la msingi la Tume ya Uchaguzi la kuratibu na kuendesha chaguzi hapa nchini. Kwa mwaka fedha 2026/2027, Programu hii ya Tume ya Uchaguzi imepanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kuendelea kutoa Elimu ya Wapiga Kura;

ii. Kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kupokea maombi ya Uhamisho na masahihisho ya taarifa za wapiga kura;

iii. Kuendesha chaguzi ndogo iwapo itatokea haja ya kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria

## PROGRAMU KUU - (PO3102): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

**142. Mheshimiwa Spika;** Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Utawala za Afisi ya Tume ya Uchaguzi inahusika na shughuli za mipango na uendeshaji wa Tume ya Uchaguzi ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Tume ya Uchaguzi kupitia Programu hii itatekeza kazi zifuatazo:

i. Kuendelea na uratibu na usimamizi wa Mradi wa Ujenzi Afisi za Tume za Wilaya za Kaskazini A, Kaskazini B, Kati kwa Unguja na Wilaya za Micheweni na Mkoani pamoja na Afisi Ndogo ya Uchaguzi Pemba;

ii. Kununua vifaa na huduma mbali mbali kwa ajili ya kuwezesha utendaji na kuleta ufanisi katika Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;

iii. Kuendelea kusomesha na kuwaendeleza kitaaluma wafanyakazi wa Tume katika kada na ngazi mbali mbali;

iv. Kuimarisha majengo ya Afisi za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**143. Mheshimiwa Spika;** ili Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iweze kutekeleza kazi zake kupitia Programu zake kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 6,511,180,000** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 5,236,770,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 1,274,410,000** ni kwa matumizi mengineyo.

## UKUSANYAJI MAPATO

**144. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 60,132,000** kupitia Fungu la 003 (Ofisi Makamu wa Pili wa Rais -Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Afisi Kuu Pemba) na Fungu 031 (Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar) kwa mchanganuo ufuatao: -

| | |
|---|---|
| Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 33,332,000 |
| Afisi Kuu Pemba | 11,800,000 |
| Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | 15,000,000 |
| **Jumla** | **60,132,000** |

**145. Mheshimiwa Spika;** kwa muhtasari, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu Matatu ya Kibajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake yenye Programu Kuu saba (**7**), kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni jumla ya **Shilingi 135,676,558,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 25,066,368,608** kwa ajili ya mshahara, **Shilingi 59,867,100,000** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 40,000,000,000** kwa miradi ya maendeleo **(Kiambatisho Nam. 5)**. Na kwa upande wa makusanyo ni **Shilingi 60,132,000.**

## HITIMISHO

**146. Mheshimiwa Spika;** kwa kuhitimisha hotuba hii kwa mara nyengine napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani na tunamuomba kwa rehema zake atuzidishie utulivu huu. Aidha, kwa dhati kabisa napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uweledi mkubwa na kusimamia haki, demokrasia na utawala bora. Namuomba Mwenyezi Mungu awaongezee hekima, busara na afya njema viongozi wetu hawa katika kuliongoza taifa hili.

**147. Mheshimiwa Spika;** namshukuru sana Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa usaidizi wake katika kuiongoza Ofisi yetu na kuhakikisha tunafikia malengo yetu kwa ufanisi mkubwa. Vilevile, natoa shukurani kwa watendaji na wafanyakazi wote wa Ofisi Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Islam Seif Salum na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Salhina Mwita Ameir ambao wameendelea kusimamia vyema mipango na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

**148. Mheshimiwa Spika;** Tunawashukuru sana washirika wa maendeleo ambao wamekuwa nasi katika shughuli zetu za maendeleo ya nchi yetu. Tumeshuhudia miradi mingi ikitekelezwa na sekta zetu kwa ushirikiano na msaada mkubwa wa kifedha, kitaalamu na vifaa wanaotupatia wenzetu hawa. Tunazishukuru sana nchi marafiki na mashirika mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, WFP, UN-Women, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu Malaria na UKIMWI, Nchi za China, India, Finland,

Japan, Oman, Umoja wa Falme za Nchi za Kiarabu (UAE), Cuba na nyenginezo. Nchi yetu itaendelea kushirikiana na washirika hawa na wengine katika kutekeleza miradi na programu mbali mbali zinazolenga kuinua uchumi wa nchi na kuimarisha ustawi wa wananchi na nchi kwa jumla.

**149. Mheshimiwa Spika;** Vilevile naomba kuchukua nafasi hii kuzishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambazo tunafanya kazi kwa pamoja katika masuala mbalimbali ya kitaifa. Kadhalika, tunazishukuru sana Taasisi, Jumuiya na Mashirika ya kitaifa pamoja na wafanyabiashara ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma kwa wananchi katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Nawaomba waendelee kushirikiana na Serikali kwa kadri hali inavyoruhusu ili kwa pamoja kuweza kufikia lengo letu la kuwahudumia wananchi kwa ubora wa hali ya juu.

**150. Mheshimiwa Spika;** pia, tunawashukuru waandishi wa habari wa vyombo vyote nchini kwa kusaidia kutoa taarifa mbalimbali za kimatukio na za kuelimisha ikiwemo mikutano yetu ya Baraza la Wawakilishi. Nawaomba waendelee kutoa taarifa kwa umakini zaidi na kwa kutumia weledi na taaluma zao bila ya kufuata utashi wa mtu au taasisi.

**151. Mheshimiwa Spika;** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 135,676,558,000** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu **7** na Programu Ndogo **14** nilizozielezea hapo awali. Mchanganuo wa fedha hizo kwa Programu ni kama zinavyoonekana katika (**Kiambatisho Nam. 6)** na kwa mafungu ni kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 003: Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais | **Shilingi** | **92,315,728,000** |
| 020: Afisi ya Baraza la Wawakilishi | Shilingi | **36,849,650,000** |
| 031: Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | Shilingi | **6,511,180,000** |
| **JUMLA KUU** | **Shilingi** | **135,676,558,000** |

**152. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.



**MHESHIMIWA HEMED SULEIMAN ABDULLA**
**MAKAMU WA PILI WA RAIS**
**ZANZIBAR**

Kiambatisho Nam. 1.

**PROGRAMU KUU NA PROGRAMU NDOGO ZA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

| Na. | KIFUNGU CHA PROGRAM | PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI |
|---|---|---|---|
| 1. | **Programu Kuu: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais: P03** | | |
| | S0301 | 1) Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | Afisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais |
| 2. | **Programu Kuu: Uratibu wa Shughuli za Serikali: P02** | | |
| | S0201 | 2) Kukabiliana na Maafa | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa |
| | S0202 | 3) Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa | Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa |
| | S0203 | 4) Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ |
| | S0204 | 5) Shughuli za SMZ Dodoma | Afisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, Dodoma |
| 3. | **Programu Kuu: Uendeshaji na Uratibu: P01** | | |
| | S0101 | 6) Uongozi na Utawala | Idara ya Uendeshaji na Utumishi |
| | S0102 | 7) Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti |

| Na. | KIFUNGU CHA PROGRAM | PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI |
|---|---|---|---|
| | S0103 | 8) Afisi Kuu Pemba | Afisi Kuu Pemba |
| 4. | **Programu Kuu: Kutunga Sheria, kupitisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali: P01** | | |
| | S0101 | 9) Kutunga Sheria, Kupitisha Sheria na Kusimamia Taasisi za Serikali | Baraza la Wawakilishi |
| 5. | **Programu Kuu: Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi: P02** | | |
| | S0201 | 10) Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | Baraza la Wawakilishi |
| | S0202 | 11) Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba | |
| 6. | **Programu Kuu:Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar: P01** | | |
| | S0102 | 12) Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Unguja | Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar |
| | S0101 | 13) Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Pemba | |
| 7. | **Programu Kuu: Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi: P02** | | |
| | S0201 | 14) Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi | Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar |

**Kiambatisho Nam. 2.**

**VIKAO VYA MASHIRIKIANO OFISI YA URATTIBU WA SHUGHULI ZA SMZ – DODOMA JULAI 2025 – MACHI 2026**

| Na. | Tarehe | Jina la Kikao | Sehemu ya Kikao | Lengo la Kikao |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 02.07.2025 | Utoro kwa wanafunzi au waajiriwa wapya wa JWTZ hususan vijana kutoka Zanzibar (Wengi wao wanatoka katika mikoa ya Kaskazini Pemba na Mjini Magharibi | Ngome – Makao makuu ya Jeshi Msalato Dodoma | Udhibiti wa Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kutoroka mara tu wanapomaliza mafunzo, hupewa mapumziko ya wiki moja au mbili kurudi katika familia na hawarudi tena kazini |
| 2. | 15.07.2025 | Udhamini wa masomo kutoka kwa wafadhili wa nchi husika | Wizara ya Elimu – Mtumba Dodoma | Zinapokuja nafasi za masomo kutoka kwa wafadhili na nchi wahisani Zanzibar hupewa nafasi za masomo lakini wanashindwa kupeleka wanafunzi na badala yake nafasi hizo hazijazwi na kukosa fursa kwa Wazanzibari |
| 3. | 17.07.2025 | Kikao cha maandalizi ya maadhimisho ya kumbukumbu ya mashujuaa yaliyofanyika 25/07 | Ofisi ya Waziri Mkuu – Relini Dodoma | Kufanya maandalizi pamoja na kusambaza kadi za mialiko na kuhakiki kila muhusika anapata mualiko |
| 4. | 17.07.2025 | Kikao cha (5) cha maandalizi ya mkutano wa 16 wa JPC kati ya Tanzania na Rwanda | Wizara ya Mambo ya Nje – Mtumba Dodoma | Kupokea taarifa ya hali ya utekelezaji wa makubaliano ya mkutano wa JPC wa 15 na maeneo mapya ya ushirikiano kati yao. |
| 5. | 17.07.2025 | Kikao cha kwanza kwa mwaka 2025/2026 cha kamati ya wataalamu ya kudhibiti deni la taifa | Wizara ya Fedha (Hazina) – Treasury Square Dodoma | Kujadili na kufanya tathmini ya maandiko ya mikopo, misaada na dhamana kama sharia namba 19(1)(2)(3) inavyosema ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya |

| Na. | Tarehe | Jina la Kikao | Sehemu ya Kikao | Lengo la Kikao |
|---|---|---|---|---|
| 6. | 19.08.2025 | Kikao cha pili kwa mwaka 2025/2026 cha kamati ya wataalamu ya kudhibiti deni la taifa | | Mikopo dhamana na misaada. |
| 7. | 22.07.2025 | Uwiano wa ajira katika sekta za Muungano hususan Wizara ya Mambo ya Ndani – Polisi, Uhamiaji | Wizara ya Mambo ya Ndani – Mtumba Dodoma | Majadiliano kuhusu mfumo bora zaidi wa mgawanyo wa ajira za muungano kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa ajira zitokanazo na Wizara ya Mambo ya Ndani. |
| 8. | 25.07.2025 | Kikao cha kamati tendaji ya Programu ya masomo ya muda mrefu ya JICA | Mtandaoni<br>(On line) | Kujadili programu hiyo ya masomo ya muda mrefu na kukubaliana orodha ya wanafunzi wa awamu ya 13. Pia kutoa taarifa ya sherehe ya kuwaaga. |
| 9. | 28/07/2025 | Kikao cha wadau kwa ajili ya kujadili maandalizi ya mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa Shughuli za mazingira<br>(e-Mazingira) | Kikao hicho kilifanyika Four points by Sheraton hotel – Arusha . | Lengo ni kujadili namna bora ya Ofisi ya Makamu wa Rais kusimamia Shughuli za Mazingira kutokana na changamoto ya ucheleweshwaji wa taarifa na mapungufu ya utekelezaji wa miradi ya mazingira nchini. |
| 10. | 29.07.2025 | Miradi ya Kimkakati na kiuchumi itakayowezesha wananchi kujiendeleza kiuchumi na kuwaondolea shida za kiuchumi | Wizara ya Fedha (Hazina) – Treasury Square Dodoma | Kutayarisha miradi bora Zaidi ambayo itawagusa wananchi moja kwa moja ambayo itawainua kiuchumi na kuwaondolea ukali wa maisha na yenye tija kwa taifa |
| 11. | 06.08.2025 | Majadiliano kuhusu sherehe za Muungano | Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira – Mtumba Dodoma | Kuangalia njia bora Zaidi ya kusheherekea siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar April 26 kila mwaka na kutokusubiri hadi ikaribie siku au kuenzi ndio shamra shamra zianze badala yake Muungano uwe endelevu kwa kufanya |

| Na. | Tarehe | Jina la Kikao | Sehemu ya Kikao | Lengo la Kikao |
|---|---|---|---|---|
| | | | | matukio mengi zaidi kila siku, Mfano elimu kutolewa ya Muungano , Makala na Maandika na Machapisho |
| 12. | 19.08.2025 | Miongozo kuhusu sherehe za kitaifa | Ofisi ya Waziri Mkuu – Relini Dodoma | Ofisi ya Waziri Mkuu imetayarisha miongozo ya Sherehe za Kitaifa kwa kushirikisha Taasisi zote kuhusu njia bora ya kusheherekea Sherehe za Kitaifa na kuachana na njia ya zamani kwa sehemu moja ya Muungano kumiliki sherehe kwa upande mmoja |
| 13. | 23.08.2025 | Msaada wa kisheria wa Mama Samia | Wizara ya Katiba na Sheria – Mtumba Dodoma | Tathmini ya kujadiliana kuhusu kampeni ya msaada wa kisheria na Mama Samia kuhusu namna bora Zaidi ya kuwasaidia wananchi kwa kuwapa huduma za kisheria bila malipo, Mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika utoaji wa huduma hiyo |
| 14. | 27.08.2025 | Sherehe ya kuwaaga wanafunzi waliopata nafasi za kusoma Japani kupitia mradi wa JICA | Protea Hotel – Dar es Salaam | Kuaga wanafunzi waliojipatia nafasi ya kusoma nchini Japan, Safari ilikua September |
| 15. | 22–24.09.2025 | Mkutano wa wataalamu wa nchi wanachama kujadili Mkataba wa ulinzi wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki | Arusha International Convention Centre (AICC) – Arusha | a) Kujadili Mkataba wa Ulinzi wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.<br>b) Kutoa msimamamo wa Tanzania juu ya Mkataba huo |
| 16. | 29.09.2025 | Kikao cha pili cha kamati ndogo ya Itifaki, Mialiko na Sherehe ya kuingiza Serikali mpya madarakani mwaka 2025 | Ofisi ya Waziri Mkuu – Magogoni Dar es Salaam | Kwa ajili ya kupitia bajeti ya kamati pamoja na kuandaa orodha ya waalikwa wa ndani na nje pamoja na kuandaa mialiko ya wageni wa ndani na nje. Aidha kuandaa majukwaa |

| Na. | Tarehe | Jina la Kikao | Sehemu ya Kikao | Lengo la Kikao |
|---|---|---|---|---|
| | | | | ya uapisho |
| 17. | 02.10.2025 | Kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Muungano na kazi zake kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar | Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira | Kuanza kujadiliana kuhusu uendeshaji wa Taasisi za Muungano ambazo zinafanya kazi katika sehemu zote mbili bara na Zanzibar Mfano, NIDA, Uhamiaji, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Posta, TRA, TANTRADE, Tume ya Uchaguzi, Mamlaka ya Hali ya Hewa, Sekretariet ya Ajira, Pamoja na ajira kwa watumishi wanaofanya kazi katika Taasisi hizo. |
| 18. | 04.10.2025 | Ucheleweshaji wa Fedha za Wabunge wa Zanzibar | Wizara ya Fedha (Hazina) – Treasury Square Dodoma | Kumekuwa na ucheleweshaji wa Fedha za mfuko wa jimbo kwa wabunge wa Zanzibar, Hivyo kikao kilijadili njia bora zaidi itakayotumika kwa wabunge wa Zanzibar kupata fedha hizo kwa haraka zaidi ili kuondoa changamoto hio kwa kuheshimika wabunge wanaotoka Zanzibar |
| 19. | 01.10.2025 | Kikao cha tatu cha kamati ndogo ya itifaki, Mialiko na Sherehe ya kuingiza Serekali mpya madarakani | Ofisi ya Waziri Mkuu – Magogoni Dar es Salaam | Kwaajili ya kutembelea sehemu zote muhimu kwaajili ya wageni waalikwa kuangalia barabara ambazo watapitia na pia kuangalia sehemu ambazo watalala Mfano. Hoteli |
| 20. | 22.10.2025 | Kikao cha nne cha kamati ndogo ya itifaki, Mialiko na Sherehe ya kuingiza Serikali mpya madarakani | Ofisi ya Waziri Mkuu – Magogoni Dar es Salaam | Kuandaa kadi za mialiko, vitambulisho, ratiba ya uwapisho na kupanga utaratibu mahususi wa kuingia na kukaa, maeneo ya matukio pamoja na kuhakikisha uwepo wa vifaa vyote muhimu kama vile PA System, Mazulia, Viti, Mahema, LED Screen Air cooler na Vifaa |

| Na. | Tarehe | Jina la Kikao | Sehemu ya Kikao | Lengo la Kikao |
|---|---|---|---|---|
| | | | | vya ukalimani |
| 21. | 12.10.2025 | Taasisi za Kidini | Wizara ya Mambo ya Ndani – Mtumba Dodoma | Taasisi za kidini na mchango mkubwa wa kuleta Amani na utulivu nchini. Hivyo zimeshauriwa kuhubiri Amani utulivu na kuleta umoja na maelewano na mshikamano |
| 22. | 27.10.2025 | Changamoto za Muungano | Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira | Kujadiliana changamoto zilizojitokeza kwa watanzania wengi kujadili katika mitandao ya kijamii neno Tanganyika badala ya Tanzania. |
| 23. | 11/11/2025 | Kikao cha kwanza cha maandalizi ya mkutano maalum wa wakuu wanchi wa Umoja wa Afrika | Kilifanyika ukumbi wa Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mtumba Dodoma | Lengo ni maandalizi ya wasilisho la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakapokuwa kwenye mkutano huo pamoja na kuweka wazi msimamo wa nchi. |
| 24. | 14/11/2025 | Kikao cha kwanza cha Kamati ya ushauri na usimamizi wa ujenzi na uendeshaji wa makao Makuu ya Mji wa Serikali | Kilifanyika mji wa Serikali Mtumba Dodoma | Lengo ni kufanya muendelezo wa kupanga mji pamoja na kupangilia bustani, kuweka eneo la kuegesha magari kutokana na uhitaji wake na pia kujadili namna nzuri ya kusimamia mji huo. |
| 25. | 18/11/2025 | Kikao cha pili cha wadau kuhusu uchambuzi wa Ada za mafunzo kwa vitendo (intership) na gharama za vibali vya kufanya biashara kwa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa Jamuhuri ya watu wa | | Lengo ni kufuatilia maagizo yaliyotolewa na Waheshimiwa makatibu wakuu, viongozi wa Tanzania, Zanzibar na Jamuhuri ya watu wa Kenya, na kujadiliana jambo la watu wa Kenya kutozwa fedha kwa wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo wa Kenya wakiwa |

| Na. | Tarehe | Jina la Kikao | Sehemu ya Kikao | Lengo la Kikao |
|---|---|---|---|---|
| | | Kenya | | Tanzania na kinyume chake. |
| 26. | 26/11/2025 | Kikao cha kamati ya kitaalamu ya kudhibiti madeni | Kikao kilifanyika ukumbi wa Hazina Dodoma | Lengo ni kujadili na kufanya tathmini ya maombi ya kuchukuwa mkopo, kupokea ada na kupewa dhamana. |
| 27. | 14/012026 | Tathmini ya matokeo ya wanafunzi waliofanya mitihani ya taifa ya kidato cha nne na kidato cha sita | Kikao kilifanyika wizara ya Elimu Mtumba Dodoma | Kufanya Tathmini kwa wanafunzi wa kidato cha nne na cha sita na kubaini changamoto zilizojitokeza katika mitihani ya taifa na nini kifanyike ili wanafunzi waweze kufaulu zaidi |
| 28. | 20/01/2026 | Usajili wa Jumuiya za kiraia zisizo za kidini | Wizara ya mambo ya ndani Dar es Salaam | Kuongeza tija kwa vikundi au vyama na kutambulika rasmini na Serikali na kuwa na vyama imara. |
| 29. | 30/01/2026 | Kudhibiti utitiri wa ving'ora | Wizara ya Mambo ya ndani Dodoma | Kutafuta namna ya kudhibiti ving'ora vya Taasisi binafsi ambazo huwa zinapiga ving'ora ya ruhusa ya Serikali na kutoa taharuki barabarani. |
| 30. | 05/02/2026 | Kuratibu na kujadili kufua tawi kubwa Tanzania Agricultural Development Bank TADB) Benki ya Maendeleo ya Kilimo Zanzibar | Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma | Kufungua Tawi kubwa la (TADB) Zanzibar kwa ajili ya kurahisisha upatikanani wa Huduma kwa urahisi zaidi |
| 31. | 13/01/2026 | Kusaini makubaliano ya ushirikiano kati ya Wizara ya Katiba na Sheria na Chuo Kikuu Dodoma | Wizara ya Katiba na Sheria Mtumba Dodoma | Kuboresha upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi ili kupata huduma za kisheria kwa haraka na ufanisi zaidi |
| 32. | 17/02/2026 | Matayarisho ya uzinduzi wa msaada wa kisheria wa mama Samia legali | Wizara ya Katiba na Sheria | Kuboresha upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi ili kupata |

| Na. | Tarehe | Jina la Kikao | Sehemu ya Kikao | Lengo la Kikao |
|---|---|---|---|---|
| | | Aid Campain | Mtumba Dodoma | huduma za kisheria |
| 33. | 20/02/2026 | Fedha za Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar | Wizara ya Fedha na Uchumi Dodoma | Kutathmini fedha za Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar kuhusu ucheleweshaji na upatikanaji wa Fedha za maendeleo ya Jimbo. |
| 34. | 24/02/2026 | Maendeleo ya Kilimo Bora Tanzania | Wizara ya Kilimo Mtumba Dodoma | Kufanya tathmini juu Sekta ya Kilimo Tanzania na mabadiliko ya hali ya hewa ili kuwa na kilimo chenye tija na matokeo bora zaidi. |
| 35. | 08/01/2026 | Kikao cha Tano cha Kamati ya Kitaalamu ya Kudhibiti Madeni (TDMC) | Ukumbi wa Hazina Dodoma | Kujadili na kufanya tathmini ya maombi ya taasisi kuchukuwa mikopo, kupokea misaada na kupewa dhamana kwa kuichakata kitaalamu juu ya faida na hasara zake kwa taifa letu la Tanzania. |
| 36 | 28/01/2026 | Kikao cha Pili cha Dharura cha Kamati ya Kitaalamu ya Kudhibiti Madeni TDMC) | Ukumbi wa Hazina Dodoma | Kujadili na kuafanya tathmini ya maombi ya taasisi kuchukuwa mikopo, kupokea misaada na kupewa dhamana kwa kuichakata kitaalamu juu ya faida na hasara zake kwa taifa letu la Tanzania. |
| 37 | 25/02/2026 | Kikao cha Sita cha kamati ya Kitaalamu ya Kudhibiti Madeni (TDMC) | Ukumbi wa Hazina Dodoma | Kujadili na kuafanya tathmini ya maombi ya taasisi kuchukuwa mikopo, kupokea misaada na kupewa dhamana kwa kuichakata kitaalamu juu ya faida na hasara zake kwa taifa letu la Tanzania.. |
| 38 | 11/03/2026 | Kikao cha Pili cha Kamati ya Wataalamu cha Maandalizi ya Maadhimisho ya Sherehe | Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma | Kufanya maandalizi ya namna sherehe hiyo itakavyofanyika, mahala, wageni watakaoalikwa |

| Na. | Tarehe | Jina la Kikao | Sehemu ya Kikao | Lengo la Kikao |
|---|---|---|---|---|
| | | ya Miaka 62 ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania | | na kuwasilisha bajeti. |
| 39 | 24-25/03/2026 | Ziara ya Kamti ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar | Mfuko wa Maendeleo TASAF, Ofisi ya Uratibu shughuli za SMZ Dodoma na Mamlaka ya Mapato (TRA) | Kujifunza namna wanavyofanya kazi na kuona Shughuli zao za uendeshaji wa kila siku. |

**Kiambatanisho No. 3.**

## Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Mishahara kwa Kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026

| S/N | JINA LA PROGRAMU NDOGO | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | | | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | | | (%) KWA MIEZI TISA | % KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | MISHAHARA | OC | JUMLA | MISHAHARA | OC | JUMLA | | |
| 1. | Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | 2,023,250,000 | 1,010,985,750 | 549,219,000 | **1,560,204,750** | 967,689,741 | 198,476,414 | **1,166,166,155** | **75** | **58** |
| 2. | Kukabiliana na Maafa | 2,176,000,000 | 739,500,000 | 931,086,847 | **1,670,586,847** | 753,172,325 | 535,334,998 | **1,288,507,323** | **77** | **59** |
| 3. | Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa | 2,018,792,000 | 241,343,250 | 1,660,216,000 | **1,901,559,250** | 270,735,970 | 1,691,285,560 | **1,962,021,530** | **103** | **97** |
| 4. | Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | 4,657,883,300 | 577,411,488 | 3,758,344,300 | **4,335,755,788** | 534,770,510 | 3,176,298,843 | **3,711,069,353** | **86** | **80** |
| | Idara ya Uhamiaji Zanzibar | 25,573,700,000 | | 19,179,000,000 | **19,179,000,000** | | 21,310,000,000 | **21,310,000,000** | **111** | **83** |

| S/N | JINA LA PROGRAMU NDOGO | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | | | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | | | (%) KWA MIEZI TISA | % KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | MISHAHARA | OC | JUMLA | MISHAHARA | OC | JUMLA | | |
| 5. | Shughuli za SMZ Dodoma | 1,299,042,000 | 412,338,000 | 596,922,510 | **1,009,260,510** | 388,628,302 | 178,255,034 | **566,883,336** | **56** | **44** |
| 6. | Uongozi na Utawala | 2,641,509,000 | 846,351,000 | 1,268,516,001 | **2,114,867,001** | 945,524,169 | 786,725,691 | **1,732,249,860** | **82** | **66** |
| 7. | Mipango, Sera na Utafiti | 551,147,700 | 202,593,000 | 197,592,900 | **400,185,900** | 160,456,765 | 51,455,288 | **211,912,053** | **53** | **38** |
| 8. | Ofisi Kuu Pemba | 1,184,676,000 | 537,960,750 | 398,733,000 | **936,693,750** | 554,021,725 | 175,876,000 | **729,897,725** | **78** | **62** |
| | **Jumla ndogo** | **42,126,000,000** | **4,568,483,238** | **28,539,630,558** | **33,108,113,796** | **4,574,999,508** | **28,103,707,829** | **32,678,707,336** | **99** | **78** |
| 9. | Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali | 34,770,000,000 | 7,537,258,884 | 14,807,434,614 | 22,480,120,736 | 7,175,380,380 | 13,285,528,490 | 20,460,908,871 | **91** | **59** |
| 10. | Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | | | | | | | | | |

| S/N | JINA LA PROGRAMU NDOGO | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | | | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | | | (%) KWA MIEZI TISA | % KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | MISHAHARA | OC | JUMLA | MISHAHARA | OC | JUMLA | | |
| 11. | Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba | | | | | | | | | |
| | **Jumla ndogo** | **34,770,000,000** | **7,537,258,884** | **14,807,434,614** | **22,480,120,736** | **7,175,380,380** | **13,285,528,490** | **20,460,908,871** | **91** | **59** |
| 12. | Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi | 6,016,500,000 | 3,871,540,489 | 624,266,138 | **4,495,806,627** | 3,247,864,535 | 339,872,592 | **3,587,737,127** | **80** | **60** |
| 13. | Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Unguja | | | | | | | | | |
| 14. | Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Pemba | | | | | | | | | |
| | **Jumla ndogo** | **6,016,500,000** | **3,871,540,489** | **624,266,138** | **4,495,806,627** | **3,247,864,535** | **339,872,592** | **3,587,737,127** | **80** | **60** |
| | **JUMLA KUU** | **82,912,500,000** | **15,977,282,611** | **43,971,331,310** | **60,084,041,159** | **14,998,244,423** | **41,729,108,911** | **56,727,353,334** | **94** | **68** |

**Kiambatanisho No. 4.**

**Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Julai, 2025 – Machi, 2026**

| S/N | JINA LA PROGRAMU NDOGO | JINA LA MRADI | FEDHA ILIYOTENGWA KWA MWAKA | | FEDHA ILIYOTENGWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA YA MIEZI TISA | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Shughuli za SMZ | Programu ya TASAF III | Wahisani | 35,000,000,000 | 26,250,000,000 | 2,140,514,254 | 8.15 | 6.12 |
| | | | SMZ | 100,000,000 | 75,000,000 | 75,000,000 | 100 | 75 |
| 2. | Mipango, Sera na Utafiti | Ujenzi wa Nyumba za Makamu wa Pili wa Rais | SMZ | 2,000,000,000 | 1,500,000,000 | 1,853,259,673 | 124 | 93 |
| 3. | Mipango, Sera na Utafiti | Uratibu wa Mfuko wa ZGFCCM | Wahisani | 204,000,000 | 204,000,001 | 204,000,002 | 100 | 100 |
| 4. | Kukabiliana na Maafa | Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Maafa | Wahisani | 130,000,000 | 114,000,000 | 111,000,000 | 97 | 85 |
| 5. | Shughuli za SMZ Dodoma | Ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Uratibu Dar es Salaam | SMZ | 550,000,000 | 550,000,000 | 0 | 0 | 0 |
| | **JUMLA** | | | **37,984,000,000** | **28,693,000,001** | **4,383,773,929** | **15** | **12** |

Kiambatanisho No. 5.

## Ukusanyaji Mapato kwa Kipindi cha Julai 2025 – Machi, 2026

| S/N | IDARA/TAASISI | FEDHA ILIYOTENGWA KWA MWAKA | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOKUSANYWA MIEZI TISA | ASILIMIA MIEZI TISA | ASILIMIA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 27,240,000 | 24,132,000 | 19,975,000 | 83 | 73 |
| | Ofisi Kuu Pemba | 7,760,000 | 5,697,000 | 4,280,000 | 75 | 55 |
| | Tume ya Uchaguzi | 60,105,647 | 59,620,000 | 156,100,000 | 262 | 260 |
| | **JUMLA** | **95,105,647** | **89,449,000** | **180,355,000** | **202** | **190** |

**Kiambatanisho No. 6.**

## MGAWANYO WA BAJETI OMPR 2026/2027

| PROGRAMU NDOGO | MSHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | RUZUKU MISHAHARA | RUZUKU OC | MAENDELEO SMZ NA WAHISANI (OC) | WAHISANI MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| FARAGHA | 1,639,384,000 | 625,992,000 | | | | | **2,265,376,000** |
| SHEREHE | 402,530,000 | 1,823,164,000 | | | | | **2,225,694,000** |
| URATIBU SMZ | 821,374,000 | 3,690,929,000 | | 32,687,600,000 | 100,000,000 | 40,000,000,000 | **77,299,903,000** |
| URATIBU DOM | 820,627,000 | 1,094,581,000 | | | 550,000,000 | | **2,465,208,000** |
| U/UTUMISHI | 1,277,480,000 | 1,533,284,000 | | | | | **2,810,764,000** |
| MIPANGO | 335,227,000 | 373,620,000 | | | | 204,000,000 | **912,847,000** |
| PEMBA | 819,588,000 | 433,290,000 | | | | | **1,252,878,000** |
| MAAFA | | | 1,040,610,000 | 1,742,020,000 | 300,428,000 | | **3,083,058,000** |
| **Jumla ndogo** | **6,116,210,000** | **9,574,860,000** | **1,040,610,000** | **34,429,620,000** | **950,428,000** | **40,204,000,000** | **92,315,728,000** |
| BARAZA LA WAWAKILISHI | 12,672,758,608 | 24,176,891,392 | | | | | **36,849,650,000** |
| TUME YA UCHAGUZI | 5,236,770,000 | 1,274,410,000 | | | | | **6,511,180,000** |
| **Jumla ndogo** | **24,025,768,608** | **35,026,151,392** | **1,040,610,000** | **34,429,620,000** | **950,428,000** | **40,204,000,000** | **135,676,558,000** |